SportPesa
TZS. 559,183,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**MAKALA MAALUM**
Namna Rais Samia alivyotafuna mfupa mgumu bei mafuta
UKURASA 19


Nyama imepanda bei sasa tufanye hivi
BUFE
MSALATO YAZALIWA UPYA
Mkataba ujenzi Uwanja Ndege wa Kimataifa ulivyofumua tabasamu
IJUMAA OKTOBA 8, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Wataalamu walia bajeti ya kijinsia msukumo uanze ngazi ya mtaani

UKURASA 11

# Nipashe
MWANGA WA JAMII
Ijumaa Oktoba 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580727
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Hatimaye chanjo ya malaria yapatikana



**WHO** yaithibitisha baada ya uchunguzi wa miaka...

*Endelea ukurasa 2*



UKURASA 2

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Hashim Issa Juma (kulia), akisindikizwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, baada ya kuachiliwa kwa dhamana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, ambako alifikishwa kwa makosa mawili ikiwamo kumchafua na kumdhalilisha Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro kwa kumwita gaidi namba moja hapa nchini na fisadi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kigogo CHADEMA kizimbani tuhuma kumwita IGP gaidi

UKURASA WA 3

## VYAMA 5 KUCHUANA USHETU NA KONDE

VYAMA vya siasa vitano vilivyosimamisha wagombea katika uchaguzi mdogo kwenye majimbo ya Ushetu na Konde, vimetakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi...

UKURASA WA 3

## BARABARA NANGURUKURU-LIWALE KUJENGWA KWA LAMI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya kutoka Nangurukuru hadi...

## TEC, BAKWATA watoa mbinu uhamasishaji chanjo corona

UKURASA 3

UKURASA WA 4

## TANZANIA KUSHIRIKI DUBAI EXPO2020

TANZANIA ni miongoni mwa nchi 191 duniani zitakazoshiriki maonyesho ya kimataifa yanayofanyika Dubai maarufu kama Dubai Expo2020...



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa mikopo ya riba nafuu kwa wateja katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, jijini Dar es Salaam jana, ambapo zaidi ya shilingi bilioni 100 zimetengwa kwa ajili ya mikopo hiyo. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi na Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara, Isaac Masusu. Habari uk.4. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MICHEZO YANGA, AZAM KUKIPIGA ARUSHA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Hatimaye chanjo ya malaria yapatikana

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limepitisha rasmi matumizi ya chanjo mpya ya malaria kwa watoto iliyokuwa kwenye majaribio tangu mwaka 2019.

Mkurugenzi Mtendaji wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus, katika taarifa yake juzi, alithibitisha kwamba chanjo hiyo inakidhi ubora wa kuikabili malaria, baada ya majaribio ya kiutafiti yaliyofanywa katika nchi za Kenya, Malawi na Ghana.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya chanjo hiyo kuonyesha mafanikio makubwa katika majaribio yaliyofanyiwa kwenye nchi za Sahara Kusini mwa Afrika.

"Hii ni historia mpya, kwa muda mrefu tulihitaji kupatikana kwa chanjo ya malaria kwa ajili ya afya za watoto na kudhibiti ugonjwa huu," alisema Dk. Ghebreyesus.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo wa WHO, chanjo hiyo iliyopewa jina la RTS,S/AS01 (RTS,S), utafiti wake uliwahusisha jumla ya watoto 800,000 huku ikionyesha mafanikio kwa wastani wa theluthi mbili.

Dk. Ghebreyesus alifafanua kuwa dira ya matumizi yajayo kwa WHO kwamba: "Kwa kutumia chanjo hizi, kuunganisha na nyenzo zingine zilizopo, zitatusaidia kuokoa maisha ya watoto 10,000 kila mwaka."

Katika taarifa yake, WHO imesema uamuzi huo ulipitishwa na bodi zake mbili za kitaalamu, moja inayohusika na kinga na nyingine mahususi kuhusu ugonjwa wa malaria.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa chanjo hizo zitakatumika katika maeneo ambako kuna athari zaidi za malaria kwa dozi nne za kinga kwa vipindi tofauti kwa mtoto kuanzia umri wa miezi mitano.

Majaribio ya utafiti huo uliofikia udhibitisho wa matumizi, yalifanyika chini ya vituo maalum na usimamizi wa wizara zinazohusika na afya katika nchi hizo tatu tajwa.

Kwa mujibu wa WHO, katika bara la Afrika hususani Kusini mwa Jangwa la Sahara, malaria inaongoza katika kuwadhuru na kuwaua watoto chini ya miaka mitano, kukikadiriwa wastani wa wanaopoteza maisha ni 260,000 kila mwaka.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza baada ya kukataa kufungua barabara yenye urefu wa kilomita 1.2, katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi jana, ambayo ujenzi wake haujakamilika kwa mujibu wa mkataba uliotiwa saini kati ya mkandarasi na serikali. Kutoka (kulia) ni Meneja wa TANROADS mkoa wa Lindi, Mlavi Efatha, Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya. **PICHA: OWM**

# Kigogo CHADEMA kizimbani tuhuma kumwita IGP gaidi

**Na Kulwa Mzee**

MWENYEKITI wa Baraza la Wazee CHADEMA, Hashim Issa (63), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akituhumiwa kwa makosa mawili likiwamo kumchafua na kumdhalilisha Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro kwa kumuita gaidi namba moja nchini na fisadi.

Issa ambaye ni mkazi wa Mbweni Kiembe Samaki Zanzibar, alipanda kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali, Yusuph Aboud.

Aboud alidai mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka mawili anayodaiwa kuyatenda Oktoba Mosi, mwaka huu maeneo ya Kinondoni 'B', mtaa wa Ufipa jijini Dar es Salaam.

Inadaiwa katika shtaka la kwanza Issa alichapisha taarifa za uongo kwa njia ya kompyuta na kusambaza katika mtandao wa YouTube kwa lengo la kumchafua na kumdhalilisha IGP Sirro. Mshtakiwa anadaiwa kuchapisha kwamba IGP Simon Sirro ni gaidi namba moja nchini na fisadi.

Katika shtaka la pili anashtakiwa kwa uchochezi, inadaiwa kwa lengo la kutengeneza chuki na taharuki kwa wananchi wa Tanzania dhidi ya IGP, alitoa maneno ya uchochezi kwamba Simon Sirro ni gaidi namba moja nchini na fisadi.

Mshtakiwa alikana mashtaka, upande wa Jamhuri haukuwa na pingamizi kwa mshtakiwa kupata dhamana na wakili aldiai upelelezi uko katika hatua za mwisho. Wakili wa mshtakiwa Alex Masaba, aliomba mahakama itoe masharti nafuu ya dhamana ili mteja wake aweze kudhaminiwa.

Hakimu Chaungu alikubali kumpa dhamana mshtakiwa kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili, watakaosaini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni tatu, wawe na barua ya utambulisho, wawe na vitambulisho vya kura au Taifa.

Mshtakiwa alitimiza masharti ya dhamana, Mahakama imemwachia kwa dhamana hadi Oktoba 28, mwaka huu kwa ajili ya kesi kutajwa.

Katika hatua nyingine, Wakili Masaba aliomba kuondoa maombi aliyowasilisha awali akitaka mshtakiwa afikishwe mahakamani.

Wakili Masaba aliwasilisha maombi hayo wakati mshtakiwa akishikiliwa na Jeshi la Polisi bila kufikishwa mahakamani.

Hakimu Chaungu alikubali kuondoa maombi hayo na kusema kwamba alikuwa ameshayapangia tarehe ya kuanza kusikilizwa.

# Mpango aonya viongozi CCM wanaopora ardhi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kumaliza migogoro ya ardhi kwenye mkoa huo.

Dk. Mpango alisema kero ya migogoro ya ardhi Mkoa wa Pwani inawahusisha baadhi ya viongozi wa chama na watumishi wa Ardhi ambao wamekuwa wakipora mashamba na viwanja vya wananchi wanyonge bila kufuata utaratibu.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa Mjini Kibaha ambapo pamoja na mambo mengine, alionyesha masikitiko kuhusiana kutokana na migogoro hiyo.

Alieleza kuwa tabia ya viongozi wa CCM kushirikiana na watumishi wa A kupora mashamba ya watu na kwamba vitendo hivyo havikubaliki.

Alisema viongozi wa CCM lazima wahakikishe wanakomesha vitendo vya dhuluma ili wanyonge waweze kupata haki zao kwa wakati na watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo watatakiwa kuchukuliwa hatua.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango alisikitika baada ya kupokea taarifa ya baadhi ya watu wakishirikiana na viongozi wa CCM kuhujumu miundombinu ya mradi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere wilayani Rufiji.

Alisema kuwa, kitendo cha watu hasa viongozi wa CCM kuwa sehemu ya kuhujumu mradi huo ni jambo baya ambalo haliwezi kuvumilika na kwamba lazima hatua zichukuliwe.

Alimpongeza Kunenge kwa kuanza kuchukua hatua dhidi ya wahalifu hao ambapo ametaka vyombo vya dola kushirikiana kwa kulinda miundombinu hiyo.

Awali alitembelea mradi wa jengo la CCM linalojengwa Mjini Kibaha kutoa maelekezo kupata taarifa sahihi na historia za kuanzamradi huo.

Dkt. Mpango aliagiza viongozi wa CCM kufanya tathimini ya mradi huo ndani ya wiki mbili ikionyesha aina ya mchoro, gharama za ujenzi mpaka kukamilika kwa mradi huo.

Aidha, alitaka tathimini hiyo ionyeshe kiasi cha fedha kilichotumika mpaka sasa, fedha zilizokusanywa na fedha zilizotumika, zilizobaki, kamati ya ujenzi na kamati ya manunuzi.

Alieleza kuwa akijiridhisha na tathmini hiyo atakuwa tayari kuchangia mifuko 500 ya saruji kwa ajili ya kuendelea ujenzi wa mradi huo, huku akitaka kuona fedha zinaendana na mradi husika.

Kwa upande wake mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Ramadhani Maneno, aliishukuru Serikali kwa juhudi zake hasa katika kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na ya kijamii.

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Ama Kasangala, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya viongozi wa dini, jijini Dar es Salaam jana, ili wawahamasishe wananchi kujitokeza kupata chanjo ya Uviko-19. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TEC, BAKWATA watoa mbinu uhamasishaji chanjo corona

**Na Gwamaka Alipipi**

VIONGOZI wa dini wamesema ili kuongeza hamasa kwa watu kujitokeza kupata chanjo ya ugonjwa wa corona, zinahitajika sauti za tamalaki zitakazowaondolea hofu Watanzania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, hadi Oktoba 5 mwaka huu idadi ya Watanzania waliopata chanjo ni 681,736 sawa na asilimia 66 ya dozi zilizosambazwa nchini.

Kutokana na hali hiyo, viongozi wa dini wamesema kunapaswa kuwapo kwa ujumbe mbalimbali za hamasa, ushawishi, pamoja na sauti za kuwaondoa hofu Watanzania juu ya dhana potofu ya chanjo ya ugojwa huo.

Walitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya viongozi wa dini juu ya uhamasishaji wa chanjo ya Uviko-19, iliyoandaliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo hayo, Katibu wa Jumuiya ya Vijana wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Othman Zuber, alisema: "Vijana wanapaswa kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona. Lakini serikali nayo inapaswa kutumia ujumbe, ushawishi na sauti za kutoa hofu ili kuwavutia watu wajitokeze kupata chanjo ya corona." Padri Paul Chobo, kutoka Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), alisema maaskofu nchini wanaamini kwenye kuchanja chajo ili kuudhibiti ugonjwa wa corona.

Alisema endapo mtu akipata chanjo ya corona anakuwa amejilinda mwenyewe pamoja na mwenzake.

"Watu wajitokeze kuchanja, elimu zaidi itolewe ili watu wahamasike kwenda kupata chanjo, viongozi wa dini tuna nafasi kubwa ya kuwaelimisha waumini juu ya umuhimu wa kupata chanjo," alisema padri Chobo.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi kitengo cha elimu kwa umma, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, Dk. Ammaberg Kasangala, alisema serikali inatambua mchango wa viongozi wa dini katika mapambano ya corona.

"Mlisaidia sana katika kupunguza hofu kwa wananchi pindi ugonjwa huu ulipoingia nchini. Tunaimani mtaendelea kuwa mabalozi ili kupunguza athari," alisema Dk. Kasangala.

Dk. Kasangala alisema kundi la viongozi wa dini lina umuhimu katika kuelimisha Watanzania juu ya kujikinga na maambukizi ya ugomvi wa corona pamoja na kupata chanjo.

Kuhusu mwitikio wa kuchoma chanjo, Dk. Kasangala alisema awali mwitikio ulikuwa kidogo lakini baadaye wizara ilipeleka wataalamu mikoani kutoa elimu ya chanjo hali iliyosaidia kuongeza idadi.

Alisema kwa sasa wizara inaandaa mkakati wa kuhamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi kupata chanjo pindi dozi ya pili itakapoingia nchini na kusambazwa maeneo mbalimbali.

# Vyama 5 kuchuana Ushetu na Konde

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VYAMA vya siasa vitano vilivyosimamisha wagombea katika uchaguzi mdogo kwenye majimbo ya Ushetu na Konde, vimetakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

Uchaguzi huo utafanyika kesho huku vyama vya CCM, ACT-Wazalendo, AAFP, CUF na NCCR-Mageuzi ndiyo vilivyosimamisha wagombea.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, aliyasema hayo jana kupitia taarifa aliyotoa kwa vyombo vya habari.

Alisema pamoja na uchaguzi huo kwenye majimbo hayo pia utaambatana na uchaguzi wa udiwani kata tatu ambazo ni Vumilia, Neruma na Lyowa.

Jaji Kaijage alisema uchaguzi huo utahusisha wapigakura 191,152 walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura na vituo 529 vitatumika kupigia kura.

"Vyama vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi huu leo vina wajibu wa kuweka mawakala katika vituo vyote vya kupigia kura, kuhesabu, kujumlisha kura na wasimamizi wa uchaguzi wamekamilisha taratibu za kuwawezesha mawakala hao na vyama vya siasa kushuhudia mchakato wa uchaguzi," alisema.

Alibainisha kuwa wajibu wa mawakala hao ni kulinda maslahi ya vyama vyao na wagombea na wakati wa utekelezaji wa majukumu yao vituoni, wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

"Upigaji kura utafanyika kwenye vituo vilivyotumika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kipaumbele kitatolewa kwa wagonjwa, watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito na kinamama wanaonyonyesha watakapofika na watoto vituoni," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa wale waliopoteza kadi za kupigia kura au kuharibika na wapo kwenye daftari la orodha ya wapigakura wataruhusiwa kutumia vitambulisho mbadala ambavyo ni pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kitambulisho cha uraia kinachotolewa na NIDA.

Pia alisema kutakuwapo na majalada ya nukta nundu kwa ajili ya watu wenye uoni hafifu na wenye ulemavu wa kuona ili kupiga kura bila usaidizi.

# PM: Barabara Nangurukuru-Liwale kujengwa kwa lami

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya kutoka Nangurukuru hadi Liwale yenye urefu wa kilomita 231 ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

Pia, Majaliwa amegoma kufungua barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 1.2 iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi kwa sababu ujenzi wake haujakamilika ikiwamo kuwekwa taa za barabarani kama mkataba wa ujenzi wake unavyoelekeza.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika eneo la Idara ya Maji, Kata ya Liwale Mjini palipotengwa kwa ajili ya ufunguzi wa barabara hiyo akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani Lindi.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza kila panapojengwa barabara na ikiwa inapita kwenye eneo la mji basi pawekwe na taa sasa hapa taa hakuna, hivyo barabara hii haijakamilika kwa hiyo siifungui naomba nikazungumze mengine pale na wananchi."

Naye, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, amesema serikali imetenga Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara ya kutoka Nangurukuru hadi Liwale ikiwa ni pamoja na kujenga makaravati ili kuiwezesha kupitika wakati wote.

Baadhi ya wakazi wa Halmashauri ya wilaya ya Kilwa na Liwale, wamemshukuru Rais Samia uamuzi wake wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa sababu itakapokamilika itachochea ukuaji wa uchumi na kwa kurahisisha shughuli za usafiri.

Akiwa njiani kuelekea wilayani Liwale, Waziri Mkuu alizungumza na wananchi katika kijiji cha Kipindimbi na Zinga Kibaoni wilayani Kilwa na kusema serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha huduma za kijamii zikiwamo za afya, maji, elimu, umeme na mawasiliano zinapatikana maeneo yote nchini.

Akizungumzia elimu, ameuagiza uongozi wa Wilaya ya Kilwa uhakikishe kuwa kati ya fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu katika halmashauri hiyo uhakikishe kijiji cha Kipindimbi kinapewa kipaumbele kwa kuboreshewa miundombinu na kuongezewa vyumba vya madarasa katika shule yao ya msingi.

Pia, Waziri Mkuu amewataka wazazi wahakikishe watoto wote wenye umri wa kwenda shule wakiwamo wa kike wanapelekwa.

Aliagiza kwa viongozi wa vijiji husasani katika maeneo ya wafugaji wahakikishe watoto wote wanakwenda shule na wawakamate na kuwachukulia hatua za kisheria wazazi wote wanaowapa watoto kazi ya kuchunga mifugo badala ya kwenda shule.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | HAWA JUMANNE SAIDI | GARI | TOYOTA WISH T 659 DRG – DAR ES SALAAM. | JODAC PROFESSIONALS | 21.10.2021 |
| 2 | ROJAS MPULULE | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA MBEYA | TULVIN INVESTMENT .CO LTD | 21.10.2021 |
| 3 | ERASTO MNDEME | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA MBEYA | TULVIN INVESTMENT .CO LTD | 21.10.2021 |
| 4 | IBRAHIM MNDEME | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA MBEYA | TULVIN INVESTMENT .CO LTD | 21.10.2021 |
| 5 | KALIMEL LIHO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA MBEYA | TULVIN INVESTMENT .CO LTD | 21.10.2021 |
| 6 | CYPRIAN KIHALALWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MKUNYWA MADIBIRA | TULVIN INVESTMENT .CO LTD | 21.10.2021 |
| 7 | DOREEN D. MAJULA | NYUMBA | MAKATABA WA MAUZIANO – GOBA DAR ES SALAAM. | SCAP TANZANIA LTD | 08.11.2021 |
| 8 | SWEDY H. SWEDY | NYUMBA | HATI – KIGOGO FRESH DAR ES SALAAM. | SCAP TANZANIA LTD | 08.11.2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# Kampuni 5 za Czech zaja kutafuta fursa uwekezaji

Na Joseph Mwendapole

KAMPUNI kubwa tano kutoka Jamhuri ya Czech zimekuja chini, kwa ajili ya kutafuta fursa mbalimbali za kuwekeza ikiwamo ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha ndege, vifaa tiba vya hospitalini na kuongeza thamani mazao.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Dk. Maduhu Kazi, alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuzungumza na ujumbe wa kampuni hizo.

Ujumbe huo uliambatana na Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani ambaye pia anawakilisha Jamhuri ya Czech, Dk. Abdalah Posi na Waziri wa Mambo ya Nje wa taifa hilo, Miloslav Stasek.

Dk. Kazi alisema kundi hilo la wafanyabaishara na wawekezaji kutoka Czech limekuwa na mazungumzo mazuri na TIC kuhusu masuala mbalimbali ya uwekezaji na wameonyesha kufurahishwa na mazingira ya uwekezaji yaliyopo.

Alisema wamefurahishwa namna Tanzania ilivyo na amani na maendeleo mazuri, kwenye ukuaji wa uchumi na biashara baada ya kuambiwa fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo.

"Baada ya mazungumzo ya awali wameonyesha nia kubwa sana kuja kuwekeza kwenye pamba na viwanda vya nguo kutakuwa na ziara itafanywa na viongozi wetu wa juu, kwenda kwao kuona namna ya kushirikiana," alisema.

Alisema wafanyabiashara hao wameonyesha nia ya kuwekeza kwenye ufundi wa ndege na baadaye kutakuwa na uhusiano utakaoanzishwa, kwenye kubadilishana ujuzi kwenye eneo hilo.

Dk. Kazi alisema wageni hao wamefurahia mazungumzo na wamevutiwa na kilimo kwenye upande wa kuongeza thamani hasa viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula.

"Kweli yamekuwa mazungumzo yenye manufaa makubwa sana na tunaamini tutaendelea vizuri kwenye eneo la biashara, swali kubwa walilouliza ni namna gani ya kujiandikisha, ili wawe wawekezaji tumewaambia taratibu za kufuata na wamezifurahia," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Nje wa Czech, Miloslav Stasek, alisema mazungumzo ya ujumbe huo na TIC yamekuwa mazuri kwa kuwa wamefahamu soko la Tanzania linahitaji nini na fursa mbalimbali, ambazo kampuni za Jamhuri ya Czech zinaweza kuwekeza.

"Kampuni zimefurahia fursa zilizopo na ukubwa wa soko la hapa na watajadiliana namna ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha ndege, teknolojia, kuongeza thamani mazao na tunaomba serikali iweke maeneo maalum ya ujenzi wa viwanda kufanikisha haya," alisema.

Kwa upande wake, Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani Dk. Abdalah Posi alisema fursa za kupata wawekezaji kutoka Jamhuri ya Zchek zinazidi kuongezeka kutokana na wengi wao kufurahishwa na mazingira mazuri yaliyopo.

"Natoa raia kwa wafanyabiashara wa Tanzania kuiona hii kama fursa ya kupata mbia wa biashara kutoka taifa hili, sekta binafsi inamchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi hivyo waone hii kama nafasi muhimu kwao kuanzisha ubia na hawa wachote uzoefu na teknolojia," alisema

Dk. Posi alisema kuna kampuni kubwa ya kutengeneza ndege, ambayo imeonyesha nia ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha ndege, kwa ajili ya soko la ulimwengu mzima na kwamba hilo likiwezekana taswira ya Tanzania kimataifa itaongezeka na kuongeza ajira nchini.

"Niseme kwamba fursa za biashara baina ya Czech na Tanzania zinazidi kukua si kwenye biashara tu hata kwenye utalii na diplomasia," alisema Dk. Posi.



Mkurugenzi wa Miradi ya USAID Tanzania, Veeraya Somvongsiri (kulia), akitoa hati ya kumiliki ardhi kwa mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Nyabula, Kata ya Luhota, wilayani Iringa, mkoani Iringa, wakati wa hafla ya ugawaji wa hati kwa wakazi wa kijijini hapo jana, ambapo karibu hati 1,300 zilitolewa. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# NMB kukopesha wakulima, wafugaji, wavuvi riba nafuu

Na Enock Charles

BENKI ya NMB imesema itaanza kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wateja wake wa sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi kuanzia hatua hiyo ilitangazwa jana jijini Dar es Salaam mwezi huu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuni, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa utekelezaji wa mpango huo utaanza Oktoba 15.

Alisema mpango huo utaanza kwa kutoa mikopo ya riba nafuu na kwamba mikopo hiyo itatolewa kwa kiwango cha riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka.

Wanufaika wa mikopo ya riba nafuu ni wakulima, wauzaji wa pembejeo, watoa huduma, wajasiriamali na wasindikaji wadogo na wa kati wanaojishughulisha na shughuli zote katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Zaidi ya Sh. bilioni 100 zimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu kwenye sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

"Benki ya NMB inachukua hatua hii ili kupanua wigo wa wadau wengi katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi kupata mikopo yenye riba nafuu ambayo itaongeza tija katika shughuli zao za kiuchumi," alisema Zaipuna.

"Mteja sasa ataweza kuwa na unafuu wa gharama ya mkopo na hivyo kujitengenezea faida zaidi. Faida hiyo inaweza kutumika kuongeza uzalishaji wa chakula, malighafi za viwanda na kuchagiza maendeleo ya viwanda nchini.

Ni matarajio ya Benki ya NMB kuwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo na wa kati katika tasnia hii wataitumia fursa hii adhimu kujipatia mikopo yenye gharama nafuu na kujiongezea kipato ili kujenga uchumi wa nchi."

Alisema benki itazingatia masharti ya utoaji wa mikopo nafuu kwa kuzingatia taratibu za ukopeshaji ikiwamo kiwango cha juu cha mkopo cha Sh. bilioni moja kwa mkopaji mmoja na kwamba mkopaji huyu anaweza kuwa mtu binafsi, chama cha ushirika, kampuni au taasisi yeyote itakayokidhi masharti ya ukopeshaji.

"Benki inatoa wito kwa walengwa kuwasiliana na mtandao wake wa zaidi ya matawi 225 yaliyo enea nchi nzima ili kupata huduma za mikopo hii ya riba nafuu.

## Tanzania kushiriki Dubai Expo2020

Na Joseph Mwendapole

TANZANIA ni miongoni mwa nchi 191 duniani zitakazoshiriki maonyesho ya kimataifa yanayofanyika Dubai maarufu kama Dubai Expo2020.

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), ilisema hayo juzi wakati ilipokutana na wanachama wa Jukwaa la Wahariri (TEF) na waandishi wa habari uliofanyika kwenye ofisi za mamlaka hiyo.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Biashara wa TanTrade, Getrude Ngwesheni, alisema maonyesho hayo yalianza tangu Oktoba Mosi mwaka huu na yameandaliwa na Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Alisema Expo ni maonyesho hayo makubwa ya kidunia ambayo hufanyika kwa miezi mitatu hadi sita na huratibiwa na Shirikisho la Maonyesho Duniani (Bureau of International Expositions-BIE).

Alisema lengo la Tanzania kushiriki maonyesho hayo ni kutumia Jukwaa la Expo2020 kutangaza na kutafuta fursa za uwekezaji, masoko ya bidhaa zinazopatikana nchini, utalii na maliasili, utamaduni na mila na desturi na kujifunza mambo mbalimbali ya kibiashara na teknolojia.

Kuhusu manufaa ambayo Tanzania itapata kwa kushiriki maonyesho hayo, alisema itatangaza lugha ya Kiswahili na utamaduni kwa washiriki wapatao 207,600 na kutangaza miradi mitatu ya kipaumbele inayovutia uwekezaji.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, bwawa la kuzalisha umeme wa megawati 2,150 la Julius Nyerere na Bandari za Bara, Zanzibar na kutoa fursa ya kujifunza kwa Watanzania zaidi ya 600 kutoka kwenye nchi zitakazoshiriki. Alisema hatua ya serikali kushiriki maonyesho hayo kutasaidia kuimarisha biashara na masoko ya bidhaa na UAE kwa bidhaa za matunda kama parachichi, mikunde, maharage, mbaazi na kunde, chai, kahawa, nyama ya mbuzi, korosho, nguo, samaki, maua na karafuu.

Alisema Tanzania ina fursa ya kuongeza mauzo ya bidhaa katika soko la UAE na Jukwaa la Expo2020 Dubai linatoa fursa kwa Tanzania kupata mikataba na kuongeza mauzo ya bidhaa za matunda.

Aidha, alisema kwenye banda la Tanzania, washiriki watakaotembelea wataona makumbusho ya kihistoria, msikiti wa Kilwa, viongozi waliopita, mnara wa askari na vivutio mbalimbali vya utalii wa Tanzania.

Alisema banda la Tanzania litajumuisha washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi watakaoonyesha mazao, bidhaa na miradi ya serikali.

Alisema kampuni za uzalishaji wa bidhaa nane na sanaa zilizothibitisha ushiriki na bidhaa 137 zilifanikiwa kuingizwa katika mfumo wa mauzo wa EXPO2020 Dubai na bidhaa hizo zitajumuisha ngozi, chai, kahawa, mkonge, korosho, viungo na bidhaa za mikono ikiwemo milango ya Zanzibar.

Alisema siku maalum ya Tanzania imepangwa kufanyika Feburuari 26, mwakani na kutafanyika kongamano la biashara na uwekezaji kwa ushirikiano wa wizara za kisekta na taasisi za sekta binafsi ili kufanikisha maonyesho hayo.

# Spika Ndugai: Bunge likikosea, likosolewe

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameuomba mhimili wa mahakama kulikumbusha Bunge pale unapobaini kuna dosari katika utungaji wa sheria au kuingilia mhimili huo. Kiongozi huyo wa Bunge alitoa rai hiyo jana wakati wa uzinduzi wa jengo la Mahakama ya Mwanzo Kibaigwa wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Alisema Bunge linaheshimu mhimili wa mahakama na inapotokea kuteleza ulimi ni bahati mbaya.

"Unajua bungeni pale tuna mchanganyiko maalum, mwingine akaamka kushoto, mwingine kulia, hata ni mimi mwenyewe, basi mnatubonyeza tu, mzee huko unakokwenda... tunarudi kwenye mstari.

"Hatupendi hata mara moja kuingilia mhimili wa mahakama na wala hatujaribu kabisa, tutajitahidi kwenda na msimamo huo.

"Hata tunapotunga sheria, mnapoona kidogo kama... basi mnatukumbusha kwa kuwa hakuna mwenye nia ya kutunga sheria mbaya, nia yetu ni kutunga sheria zinazotekelezeka, nzuri zinazoweza kuiongoza nchi yetu vizuri sana," alisema.

Spika Ndugai pia aliwataka watendaji wa serikali kuheshimu uamuzi wa mahakama ili mlolongo wa haki ukamilike.

"Wiki mbili zijazo tutaenda na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria mahali, ambapo mahakama ilishamaliza mambo yake lakini wananchi wale wanavyolia haki yao haijatekelezeka unaweza kutoa machozi, kwa hiyo mahakama ikishatoa haki, yule anayebisha aende kwa mchakato wa mahakama kukata rufani," alisema.

Kuhusu jengo hilo, alisema Kibaigwa ni Mamlaka ya Mji Mdogo na kinachofuata ni kuwa na jimbo linalojitegemea, Halmashauri ya Wilaya na mji.

"Jengo hili linaona tunakoelekea, hizi ndio sifa zenyewe watakapoangalia mahakama ni balaa balaa! Kuna chemba mbili, Kibaigwa tunapenda maneno maneno, sasa ndani kwenye jengo kuna mahakama mbili, yaani hapa pamekamilika, kusafirisha mashahidi gharama kuwapeleka Kongwa na kuwarudisha kwa mwananchi ambaye uchumi wake ni mdogo, ni kazi sana. Sasa hivi gharama ni mguu wako. "Yaani ninasubiri kwa hamu nione kindumbwe ndumbwe na wa kwanza mnaotakiwa kufaidika na huduma hii ni kinamama, yaani ukipigwa kofi tu breki ya kwanza hapa, mkifika huko waambieni 'kaja Jaji Mkuu mwenyewe, wewe si umezoea kunipiga piga', aache mahakama isije ikamwanzia yeye, ukatili wa kijinsia tuache na wale wanawake wanaoonea wanaume breki ni hapa," alisema.

Spika Ndugai ambaye ni Mbunge wa Kongwa, alibainisha kuwa baadhi ya wanaume wanaonewa na wanawake kwa "kufinywafinywa" na wananyamaza, sasa mahakama imekuja na ukombozi kwao.

Akizungumza baada ya kuzindua jengo hilo, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Jumaa, alishauri umuhimu wa usuluhishi na upatanishi hasa kwa wafanyabiashara.

"Ninyi ni wafanyabiashara, mara nyingi shughuli za biashara huwa hazipendi upotezaji wa muda mwingi mahakamani, kwa bahati nzuri Katiba yetu inaruhusu suluhu, inasema nia ya Katiba ni pamoja na kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika na migogoro," alisema.

Alisema wakifanya suluhu, wanapunguza mashauri mahakamani na hawapotezi muda wa kuzalisha, kufanya kazi na kutoa huduma.

"Bahati nzuri Spika na Bunge lake wameshatunga sheria kuhusu usuluhishi mwaka juzi, ambayo inatutaka zaidi kuegemea kwenye usuluhishi halafu sisi ni Watanzania wote, na Katiba yetu inasema tunajenga nchi moja inayozingatia udugu na amani, na udugu ni sehemu ya usuluhishi, unapokuja mahakamani pengine ni mwanzo wa uadui na jirani yako," alisema.

Jaji Mkuu alisema soko katika karne ya 21 ni tofauti na soko la karne ya 20 kwa kuwa la sasa ni kubwa zaidi na kuwataka kuwa imara kwenye mitandao ili kupata masoko.




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kulia), akizungumza wakati wa kufungua kikao kazi cha pamoja kati ya uongozi wa serikali na mashirika ya Umoja wa Mataifa, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) hapa nchini, Zlatan Milisic. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yakutana na mashirika ya UN

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imekutana na Mashirika ya Umoja wa Kimataifa (UN) yanayofanya kazi zake nchini kujadili masuala mbalimbali na kutathmini Malengo ya Maendeleo Endelevu (MDG) ya kidunia yaliyopo kwenye mpango wa pamoja.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha pamoja kati ya serikali na mashirika hayo jijini hapa.

Alisema mipango itakayojadiliwa inakuwa ni sehemu ya malengo yatakayoingia kwenye bajeti kuu ya serikali ya 2022/23 na Mpango wa serikali wa miaka mitano.

Tutuba alisema serikali itaendelea kushirikiana pamoja na kufanya kazi na mashirika ya kimataifa na inatambua mchango wao mkubwa kwa Tanzania kwa kuchangia kufikia uchumi wa kati. Alisema kikao hicho kinashirikisha baadhi ya Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali nchini kwa lengo la kujadiliana kwa pamoja ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Kwa sasa kuna mashirika 22 ya kimataifa yanayofanya kazi hapa nchi kwa lengo la kusaidia miradi ya maendeleo kwa Tanzania Bara na Visiwani, tunathamini mchango wa mashirika haya ya kimataifa katika hali ya ukuaji wa uchumi hapa nchini mpaka kufikia uchumi wa kati hivyo wao ni miongoni mwa wadau waliofanikisha malengo hayo," alisema.

Alisema watapitia kwa pamoja mpango mpya wa maendeleo ambao umejikita kwenye sekta ya afya na uhimilivu wa matatizo yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mpango huo. Kadhalika, alisema watajadiliana kuhusu malengo ya ukuaji wa uchumi hapa nchini pamoja na haki za binadamu na usawa wa jinsia. Kwa upande wake, Mratibu Mkaazi wa UN Tanzania, Zlatan Milisic, aliishukuru serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuonyesha ushirikiano na mashirika ya kimataifa.

Milisic aliahidi kuendeleza ushirikiano huo kuwashukuru kwa kuendeleza vikao kazi vya pamoja ambavyo vitasaidia kujadiliana malengo yaliyotarajiwa.

Alisema kupitia vikao hivyo na wao wanafanikiwa kupata malengo ya nchi yaliyokusudiwa kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wake.

## Jamii yaombwa msaada elimu wenye ulemavu

**Na Enock Charles**

JAMII imeombwa kujitolea kwa hali na mali ili kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa kuboresha mazingira yao ya kujifunzia.

Imeelezwa kuwa kwa kufanya hivyo watafikia malengo na ndoto zao za maisha kama ilivyo kwa wengine ikiwamo kupata elimu bora.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kukabidhiwa madarasa ya shule msingi ya viziwi Buguruni jijini Dar es Salaam jana, yaliyopakwa rangi na Kampuni ya Kansai Plascon, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kuhudumia Viziwi Tanzania, Yassin Mawe, mbali na kuishukuru kampuni hiyo kwa msaada huo, aliwaomba wadau wengi kujitokeza kusaidia shule za viziwi kwa kuwa zimekuwa na uhaba wa misaada ikilinganishwa na aina nyingine za ulemavu.

"Ulemavu wa kusikia ni aina ya ulemavu usioonekana kirahisi mpaka kwa kutumia vipimo maalum, hata wadau wanaojitokeza ni wachache. Kwa kuungwa mkono na Kampuni ya Kansai Plascon kupaka rangi majengo yetu ya shule kwetu sisi wametusaidia kwa kiasi kikubwa kwa sababu huko nyuma tulikuwa tunafanya, lakini hatufikii malengo kutokana na ukosefu wa fedha," alisema Mawe.

"Wametoa mchango wao mkubwa kwa jamii kuna ile Public Private Patnership ndiyo tupo hapa katika mstari mmoja kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapata elimu yao ili wawe na fursa sawa kama wengine ambao hawana ulemavu kila mtu apate keki ya Taifa," aliongeza Mawe.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Plascon Tanzania, Hussein Jamal, alisema kampuni hiyo ilitoa takriban lita 1,600 za rangi kwa shule hiyo na kuahidi kutoa lita 1,000 katika awamu nyingine ya kupakwa rangi shule hiyo ambazo zitatumika kupakwa katika mapaa ya shule hiyo na sehemu za kulala wanafunzi ili kuzifanya kuwavutia zaidi wanafunzi hao.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Yahya Maftah, kwa msaada huo ambao alisema umeongeza ari ya wanafunzi kusoma kutokana na maboresho yaliyofanyika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tumewasikia watoa elimu sasa tuchanje

**UTARATIBU** wa kuwaendea wananchi kuwapa elimu na kuwahamasisha kuhusu chanjo ya corona umeonekana kuongeza chachu ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo, baada ya idadi ya wanaochanja kuongezeka kwa kasi. Hali hiyo inathibitishwa na takwimu mpya zilizotolewa na serikali juzi, zikionyesha kuwa hadi kufikia Oktoba 5 mwaka huu, jumla ya watu 681,736 wamepatiwa chanjo hiyo, sawa na asilimia 66 ya dozi zilizosambazwa nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, katika taarifa yake, alibainisha kuwa serikali kupitia kamati zake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea kuhakikisha elimu ya namna ya kujikinga na utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa huo inaendelea kutolewa kwa wananchi.

Alisema kuanza kwa kampeni ya jamii shirikishi na harakishi nchini kumesaidia kuongeza hamasa na mwitikio wa wananchi kupata chanjo, ambapo idadi ya wanaochanja sasa imepanda zaidi ya mara 10. Kwamba mafanikio haya ya kampeni yanatokana na kuongezeka kasi ya uelimishaji wa wadau katika sekta mbalimbali ikiwamo Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na idara yake ya Habari (Maelezo), wasanii wa sanaa zote, makundi mbalimbali ya kijamii yakiwamo ya vijana, wanawake, wazee, wanamichezo, vyombo vya dini na madhehebu mbalimbali na wanasiasa.

Aliongeza kuwa suala la kuhamasisha wananchi kwa kwenda nyumba hadi nyumba limesaidia kuongeza kasi ya utoaji chanjo, huku vituo vya kutolea huduma hiyo vikiongezeka kutoka 550 hadi kufikia 6,784 vinavyotoa chanjo nchini.

Pia alibainisha kuwa Oktoba 4 mwaka huu, serikali ilipokea shehena ya chanjo za Sinopharm na kwamba inatarajia kupokea shehena ya pili leo na kufanya jumla ya chanjo zote zilizopokewa kuwa 1,065,000. Alisema baada ya taratibu za uhakiki kukamilika, usambazaji utaanza na zitawafikia wananchi katika vituo vyote ambavyo kwa sasa vinatoa huduma ya chanjo huku elimu ikiendelea kutolewa na upokeaji chanjo utaendelea kuwa wa hiari kama ilivyoelekezwa na Rais Samia Suluh Hassan.

Kwa mujibu wa Dorothy, kutokana na uelimishaji na mwitikio mkubwa wa wananchi kupata chanjo, baadhi ya mikoa imemaliza mgawo wa chanjo za awali na imekuwa ikiomba mikoa ya jirani.

Kutokana na jitihada hizo za serikali, tunawahimiza wananchi waendelee kujitokeza kwa wingi na kuwasikiliza wataalamu wa afya wanaotoa elimu na uhamasishaji kisha wachanje.


Taarifa za wataalamu wa wizara hiyo wanaofanya uhamasishaji na chanjo kwamba kuanzia Oktoba 4, mwaka huu kasi ya kuchanja imeongezeka na kwamba takribani watu 44,000 wanachanja kila siku nchini.

Tumaamini kuwa Watanzania wengi wanawasikiliza watoa elimu na kuwaelewa kuhusiana na athari za corona na hatua za kuchukua ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo hatari. Hatua sahihi ya kuwakinga dhidi ya maambukizi ni kuchanja kwa kuwa mtu akichanja anakuwa amepunguza makali ya ugonjwa huo hata kama atapatwa tena na virusi.

Wataalamu wanasema mtu aliyechanja hata kama ataambukizwa tena hawezi kupatwa matatizo makubwa tofauti na ambaye hakuchanja kwa kuwa kuna uwezekano wa kufa au kufikia hatua ya kulazwa chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) na kuwekewa Oksijeni.

Inaelezwa kwamba katika mataifa ya Ulaya wananchi wamechanja kwa zaidi ya asilimia 76, na ndiyo maana sasa wanajazana kwenye viwanja vya michezo. Kuongezeka kwa wanaochanja kunamaanisha kwanza elimu inayotolewa inasaidia kuondoa taarifa za upotoshaji zinazotolewa na watu wachache wasioitakia mema nchi yetu. Hivyo tunawahimiza wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kuchanja, hivyo kujilinda na kuwalinda wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kinamama jamani fanyeni biashara zenu hivi kidigitali

Na Sabato Kasika

**BIASHARA** na matangazo ya karne ya 21 yanategemea teknolojia, kutokana na ukweli kwamba kwa sasa jamii inaishi katika ulimwengu wa kidigitali, hivyo kila kitu hakina budi kufanywa kidigitali.

Mtu anaweza kuwa na biashara au kampuni inayotoa huduma ama bidhaa nzuri, lakini asipofanya bidii kujitangaza kwenye mitandao ya kijamii, anaweza kuzidiwa na watu ambao huduma zao hazina ubora zaidi yake.

Kwa ujumla ni kwamba, kujitangaza au kutafuta masoko kimtandao ni njia rahisi na isiyo gharama kuwafikia watu wengi zaidi. Ndivyo wanawake wanakumbushwa kwenye mjadala wa kilinge cha simulizi.

Wanawake hao kutoka asasi mbalimbali za kiraia, walikutana hivi karibuni jijini Dar es Salaam, katika kilinge hicho kilichoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kujadili jinsi wanavyoweza kutumia mitandao hiyo kutangaza shughuli zao.

Kilinge hicho kilihusisha wanawake ambao bado ni vijana na watu wazima, kilijadili kwa kina manufaa ya kufanya biashara kidigitali, lakini pia changamoto zitokanazo na matumizi ya mitandao.

Pamoja na hayo, wanakumbushwa kuwa siku hizi mtu akitaka msaada wa jambo fulani, wazo la kwanza kumjia ni kushika simu yake na 'kuperuzi' kuhusu akitakacho na ndipo huweza kukutana na majibu ya suala alitakalo mtandaoni.

Kwa maana hiyo, jambo ambalo wanatakiwa kuzingatia, ni matumizi sahihi ya mitandao, badala ya kuitumia kuweka vitu ambavyo haviwezi kuwasaidia kupiga hatua za kimaendeleo.

Maelezo hayo yanaonyesha ni jinsi gani wanatakiwa kwenda na wakati katika karne hii ya 21, kwani katika kilinge hicho, inabainika kuwa makundi hayo mawili ya vijana na watu wazima, kila moja lina changamoto yake.

Baadhi ya vijana wanawake, wanatuhumiwa kutumia mitandao vibaya, kwa kuwapo vitu visiyo na maana badala ya kuitumia kutangaza biashara zao ili waweze kufikia maendeleo wanayoyataka.

Upande wa wanawake, watu wazima wao inaelezwa kuwa hawataki kutumia mitandao wakiamini kwamba ni uhuni au wanatingwa na majukumu ya nyumbani na kusababisha wapitwe na mambo mengi.

Kikubwa wanachokumbushwa ni kwamba, wao kama wanawake, ni lazima wawe sehemu ya suluhisho la kuondoa umaskini kwa kutangaza biashara zao kwenda mitandao ili wapate wateja wengi.

Binafsi ninaamini kwamba, kama kila kundi litazingatia kile kilichojadiliwa kwenye kilinge cha simulizi, wanaweza kunuifaika na mitandao katika kutangaza biashara wanazofanya kwenye maeneo yao.

Wanakumbushwa kuwa, karibu kila mtu yuko Facebook au Instagram, na kwamba, soko liko huko, kwa kuwa ndiko watu waliko, hivyo jambo la kufanya ni wanawake hao kupeleka biashara zao huko.

Inabainishwa kwamba, ni suala la kitu gani cha kuposti kwenye mitandao, ndipo tatizo lilipo, lakini kutokana na kile ambacho wamejifunza, ni wazi wanaweza kupiga katika biashara zao iwapo watazingatia kilichojadiliwa katika kilinge.

Hivyo, ninaamini kuwa kilichobaki sasa ni kila kundi kuangalia ni wapi linakwama kutumia mitandao ya kijamii kutangaza biashara, ili libadilike na kuchukua hatua sahihi katika kupiga hatua kwenda mbele.

Jambo la kuzingatia ni kwamba, mitandao ya kijamii ni majukwaa tofauti tofauti yenye maudhui na makundi ya watu tofauti, hivyo ni muhimu kulifahamu hilo ili kutambua kipi cha kufanya ukiwa kwenye hayo majukwaa.

Inaelezwa kuwa, ipo mitandao ambayo ina mfumo wa kukuwezesha mtu kuweka biashara yake kwenye ramani, ili watu wa karibu na eneo la mfanyabiashara waweze kumuona wakitafuta huduma au bidhaa.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TAARIFA KWA UMMA

## UNUNUZI, UUZAJI NA USAJILI WA MAGARI BILA KUFUATA TARATIBU NA UHAKIKI KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO

Kwa kuzingatia Kifungu Na. 117, 119 na 200 vya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004, ikisomwa kwa pamoja na Kifungu Na. 11 cha Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuufahamisha na kuukumbusha umma kufuata taratibu zilizoanishwa kwa mujibu wa sheria wakati wa ununuzi, uuzaji na uhamishaji umiliki wa magari kabla ya kupata usajili wa magari hayo. Hapa siku za karibuni tumebaini ukiukwaji wa sheria katika maeneo yafuatayo:-

1. **Magari Yaliyoingizwa Nchini kwa Msamaha wa Kodi**
   Mtu yeyote anayehitaji kuuza, kununua au kubadili umiliki wa gari ambalo lina msamaha wa kodi, anapaswa kufika ofisi ya karibu ya Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya kujua kiasi cha kodi anachopaswa kulipa kabla ya kununua na kubadili umiliki. Kutumia gari hilo bila kufuata utaratibu huu ni kosa kisheria.

2. **Magari Yaliyoingizwa Nchini kwa Hati ya Muda Mfupi (Temporary Import)**
   Magari yote yalioyoingizwa nchini kwa hati ya muda mfupi kwa lengo la utekelezaji wa shughuli maalum iliyoidhinishwa kwa mujibu wa sharia kama iliyotajwa katika Kifungu Na. 136 cha sheria iliyotajwa hapo juu, yakiwemo magari binafsi, yamepewa muda maalum wa ukamilishaji wa shughuli hiyo ya kuwepo kwao hapa nchini. Wananchi wote pamoja na waigizaji wa magari hayo, wanatahadharishwa kuwa muda huo ukiisha yanapaswa kurudishwa nchi yalikotoka. Kuendelea kutumia magari hayo nje ya muda ulioanishwa ni kosa kisheria.

Aidha, yeyote atakayehitaji kuuza, kununua au kubadili umiliki wa magari hayo ni lazima afike ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya uhakiki na kupewa taratibu za kufuata,

3. **Magari Yaliyoingizwa Nchini Kinyume na Sheria**
   Haya ni magari yaliyoingia nchini bila ya kufuata taratibu, ama kwa njia ya magendo ama Transit. Tunawakumbusha wote wanaoingiza magari nchini kufuata taratibu zilizowekwa ikiwemo kupita katika njia zilizoainishwa.

**Kwa mantiki hiyo:** Wananchi wote wanashauriwa kuwa wanapotaka kununua gari yoyote, kudai nyaraka zilizotumika kuingiza gari hiyo nchini. Aidha wanunuzi hao wanatakiwa kuhakiki nyaraka hizo katika ofisi za TRA zilizo karibu.

**“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi**
**Idara ya Huduma na Elimu kwa Walipakodi**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

216501202

## TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatarajia kufanya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu mbalimbali vya ofisi kwa njia ya mtandao. Mnada huo utafanyika siku ya Alhamisi ya tarehe 21 Oktoba, 2021 kuanzia saa 6:01 usiku hadi saa 7:00 mchana.

Ili kushiriki mnada huo, tembelea tovuti ya TRA ambayo ni www.tra.go.tz kuanzia tarehe 8 Oktoba, 2021 ili kuona bidhaa zitakazouzwa. Aidha, wanunuzi wanaweza kufika katika vituo ambavyo bidhaa hizo zinapatikana ambavyo ni Chuo cha Kodi (ITA) kilichopo Mikocheni eneo la Viwanda Dar es Salaam, Ofisi ya TRA Mkoa wa Iringa na Ofisi ya TRA Mafinga – mkoa wa Iringa kwa ukaguzi kabla ya kushiriki mnada husika.

**MASHARTI YA MNADA PENDEKEZWA**

1. Bidhaa itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
2. Malipo yote yatakuwa kwa fedha taslimu ambapo malipo ya awali ya kiwango cha asilimia 25 kitalipwa ndani ya saa 24 kulingana na taratibu za uendeshaji wa minada. Kiwango cha asilimia 75 kitalipwa ndani saa 48. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi na malipo ya awali yaliyolipwa hayatarudishwa.
3. Mnunuzi atalazimika kuondoa vifaa chakavu alivyoshinda mnadani ndani ya siku tatu (3) baada ya kukamilisha malipo ya asilimia 100.
4. Ruhusa ya kuangalia vifaa imetolewa kwa siku 14 kabla ya tarehe ya mnada.
5. Mnada utaanza siku ya tarehe 21 Oktoba 2021 saa sita (6) na dakika moja usiku na kuisha hiyo hiyo saa saba (7) mchana.
6. Vigezo na masharti kuzingatiwa.

**Pamoja Tunajenga Taifa Letu**
**Imetolewa na**

**KAMISHNA MKUU**

2165013O2

## Ushauri wa FAO kilimo Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Qu Dongyu.

Mazungumzo hayo yalifanyika jana makao makuu ya shirika hilo yaliyoko Roma, Italia.

Dk. Qu Dongyu aliishauri Tanzania kuchagua zao moja la kilimo miongoni mwa mazao mengi yaliyopo kwa ajili ya kuitangaza Tanzania kimataifa na kwamba FAO iko tayari kusaidia ujuzi na kuijengea uwezo Tanzania kufikia lengo hilo.

Aliongeza kuwa kwa sasa FAO imeanzisha jukwaa maalum la kuwawezesha wanawake na vijana kunufaika na Sekta ya Kilimo kutokana na utafiti kuonyesha kuwa wanawake wengi katika nchi zinazoendelea wanajihusisha na kilimo.

Balozi Mulamula yuko Roma kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Tatu wa Mawaziri wa Mambo ya Nje kutoka nchi za Afrika na Italia pamoja na kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Amani.

## Bashe abaini tatizo wakulima Rukwa

**Na Mwandishi Wetu,** KALAMBO

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amewataka wakulima mkoani Rukwa, kujikita katika kilimo cha mazao mengi ya biashara, ili wajikwamue na vikwazo vya kuporomoka kwa bei ya mahindi katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Amewahimiza kulima mazao ya biashara ikiwamo soya na ngano kuliko kutegemea mahindi pekee kama zao la chakula na biashara.

Alisema hayo juzi katika ziara yake mkoani Rukwa, huku akisisitiza kuchukua hatua kali, dhidi ya viongozi wa vyama vya ushirika wanaofanya ubadhirifu.

Bashe aliwataka viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Ufipa (UCU) kutowadai wananchama wake kulipa deni la Sh. milioni 900, ambalo lilisababishwa na baadhi ya viongozi wa chama hicho, ambao walichukua mbolea ya mkopo kwa matumizi binafsi.

Aliwaagiza viongozi wa UCU kuwa na taratibu za kumtambua wakala aliyekikopesha chama hicho, pembejeo hizo za kilimo.

Katika ziara hiyo, Bashe alibaini ubadhirifu unaofanyika katika Wilaya ya Kalambo, ambapo baadhi ya wakulima wanalazimishwa na wakopeshaji kuwalipa madebe 18, sawa na magunia matatu ya mahindi kwa mfuko mmoja wa mbolea aina ya DAP, wenye thamani ya Sh. 70,000.

"Gunia hilo moja linauzwa kwa Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) Kanda ya Sumbawanga kwa Sh. 50,000... haiwezekani mkulima awe na deni la Sh. 70,000 halafu adaiwe magunia matatu ya mahindi, sawa na Sh. 150, 000, huu ni wizi na dhuluma kwa wakulima," Bashe alionya.

# Wafugaji waelekezwa maeneo ya kulisha

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Judith Nguli, amewataka wafugaji kufuata sheria na utaratibu, ikiwamo kuzingatia maeneo ambayo yametengwa kwa ajili malisho, ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kati yao na wakulima.

Alisema, mtindo wa wafugaji hao kuhama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili yao na kwenda kuishi sehemu ambayo hawajatengewa, unaweza chimbuko la migogoro kati ya makundi hayo mawili.

Nguli alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na viongozi wa wafugaji kwa lengo la kudumisha amani wilayani mwake kwa kuwa makundi hayo kila moja lina umuhimu wake kwa amani na maendeleo ya Liwale.

"Mtindo wa kuhama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili yenu na kwenda kuishi maeneo ambayo hamjatengewa, unaweza kusababisha migogoro kati yenu na wakulima, hivyo acheni mtindo huo," alisema Nguli.

Alisema, kinachotakiwa ni wafugaji na wakulima kuendelea kuimarisha amani na utulivu miongoni mwao wakati serikali ikiweka mikakati ya kuhakikisha inaboresha huduma mbalimbali ikiwamo ujenzi wa mabwawa ya maji.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliwataka viongozi wa vijiji ambavyo vina wafugaji wasitoe vibali kwa wafugaji wapya, badala yake washughulikie kero ambazo zinaweza kuleta kusababisha wakulima na wafugaji wakahasimiana.

"Kinachotakiwa ni viongozi wa vijijini kuangalia kama kuna changamoto miongoni mwa wakulima na wafugaji katika maeneo yao wazitafutie ufumbuzi ili makundi yote yaendelee kuishi kwa amani," alisema.

Ofisa Mifugo wa wilaya hiyo, Bernard Kivamba alisema, Liwale ina ng'ombe 30, 689, mbuzi 11, 797 na kondoo 2, 462, akifafanua kuwa Kijiji cha Kimambi ndicho kinachoongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi zaidi.

Kijiji cha Kimambi kina ng'ombe 14,000 kati ya hao 30, 689, na sasa serikali inatarajia kujenga bwawa la kunywesha maji mifugo mingine lenye thamani ya Sh. milioni 480," alisema Kivamba.

Ofisa Mifugo huyo, alifafanua kuwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022, serikali imetenga Sh. milioni 480 ambazo zitatumika kujenga bwawa hilo la kunyweshea mifugo katika Kijiji cha Kimambi.

Aidha, alisema, ofisi yake imekuwa ikijitahidi kuhakikisha Liwale haina migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kushirikisha makundi hayo kila linapotaka kutokea jambo linaloweza kusababisha uhasama.

Kiongozi wa wafugaji wilayani humo, Lugora Uporo, ameahidi kushirikiana na serikali ya wilaya hiyo kuwa atahamasisha wenzake kutokuwa chanzo cha migogoro kati yao na wakulima.

"Tutaendelea kushirikiana wote kama Watanzania, ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anaishi kwa amani na utulivu na kufanya shughuli zake za maendeleo ikiwamo kilimo na ufugaji,"




Maofisa wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Meneja Masoko na Mawasiliano Grace Majige (kulia) na Meneja wa Tawi la TCB Mpanda, Julius Mlanga (wa pili kulia), wakikabidhi sehemu ya mabati bando 15 yenye thamani ya 5.4m/- kwa Ofisa Elimu wa Mkoa wa Katavi, Dk. Elipidius Baganda (wa pili kushoto), yaliyotolewa msaada na benki hiyo kwa ajili ya kupaua madarasa mawili ya Shule ya Msingi Katavi, Manispaa ya Mpanda mapema wiki hii. Kushoto ni Mstahiki Meya wa Mpanda, Haidari Sumri na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Wailes Kibona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SGA yaunga mkono upimaji wa VVU

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA imeanzisha mpango wa upimaji wa virusi vya UKIMWI mahali pa kazi kwa wafanyakazi, hafla iliyozinduliwa katika makao makuu ya kampuni hiyo hivi karibuni.

Uzinduzi huo uliendeshwa na maofisa kutoka Chama cha Waajiri nchini (ATE), PSI Tanzania, Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) pamoja na maofisa kutoka Wizara ya Afya, ambapo uongozi wa kampuni hiyo ulipewa vifaa ambavyo wafanyakazi watapata fursa ya kujipima kwa hiari.

Uongozi wa kampuni hiyo unatarajiwa kuhifadhi vifaa hivyo vinavyotarajiwa kutatoa mwamko kwa waajiriwa kujipima wenyewe wawapo majumbani mwao ili kujua hali zao kiafya kuhusiana na masuala ya VVU na UKIMWI kwa ujumla.

Akikabidhi vifaa hivyo, mwakilishi wa ATE katika hafla hiyo Hellen Mkwizu, alisema kuwa ATE inakusudia kuwezesha waajiri kujali afya za wafanyakazi wao kwa kupima hali zao kiafya ili waweze kujitunza pale wanapobaini wako salama au wachukue zinazostahili watakapojijua wameathirika.

Alitoa rai kwa waajiri wengine kuiga mfano wa SGA utakaowawezesha wafanyakazi wao kujua hali zao na kuyalinda maisha yao.

"Lengo la serikali kupitia Wizara ya Afya ni kufikia takwimu za 95:95:95, ambayo ni asilimia 95 ya kubaini walioambukizwa VVU, asilimia ya waliogundulika kuwa na VVU kupata matibabu na asilimia 95 ya walioathirika kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs)," alisema.

Aliongeza kuwa ni matumaini yake kuwa mpango huo ulioanzishwa na SGA, utakuwa wa manufaa makubwa kwa wafanyakazi wake.

Mkurugenzi wa PSI Tanzania, Ajuae Hassan, aliishukuru SGA kwa kuchukua hatua ya upimaji mahali pa kazi na kuwa mwajiri wa mfano katika mpango wa kupima maeneo ya kazi.

"Kampuni ya ulinzi ya SGA imethibitisha kuwa ni kampuni ya mfano inayoongoza si kama mwajiri mkubwa hapa nchini bali pia kwa kujali afya za wafanyakazi wake na mfano hai ni kukubali kuzindua mpango huu," alisifu.

Kampuni ya ulinzi ya SGA imeajiri zaidi ya wafanyakazi 6,000 kupitia mtandao wake ulioenea nchi nzima. Kampuni hiyo ya ulinzi ilianza shughuli zake nchini mwaka 1984, wakati huo ikijulikana kama Group Four Security.

Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, Eric Sambu, aliwakaribisha washirika katika mpango huo ambayo kampuni yao ilipata fursa ya kuandaa uzinduzi wake.

"Siri kubwa ya mafanikio yetu inatokana na uongozi wa kampuni kujali ustawi wa wafanyakazi wetu ikiwamo kujali afya zao wawapo kazini, kupitia mpango huu, kila mfanyakazi atapata fursa ya kujua hali yake ya afya kwa na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa matokeo atakayopata baada ya kujipima," alisema.

Meneja wa Afya na Usalama wa SGA, Dickson Webi, alisema afya njema na usalama wa kutosha kwa wafanyakazi vimeisaidia kampuni hiyo kufikia malengo yake ya mafanikio inayojiwekea.

## Ushauri wa FAO kilimo Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Qu Dongyu.

Mazungumzo hayo yalifanyika jana makao makuu ya shirika hilo yaliyoko Roma, Italia.

Dk. Qu Dongyu aliishauri Tanzania kuchagua zao moja la kilimo miongoni mwa mazao mengi yaliyopo kwa ajili ya kuitangaza Tanzania kimataifa na kwamba FAO iko tayari kusaidia ujuzi na kuijengea uwezo Tanzania kufikia lengo hilo.

Aliongeza kuwa kwa sasa FAO imeanzisha jukwaa maalum la kuwawezesha wanawake na vijana kunufaika na Sekta ya Kilimo kutokana na utafiti kuonyesha kuwa wanawake wengi katika nchi zinazoendelea wanajihusisha na kilimo.

Balozi Mulamula yuko Roma kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Tatu wa Mawaziri wa Mambo ya Nje kutoka nchi za Afrika na Italia pamoja na kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Amani.

## Bashe abaini shida wakulima Rukwa

**Na Mwandishi Wetu,** KALAMBO

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amewataka wakulima mkoani Rukwa, kujikita katika kilimo cha mazao mengi ya biashara, ili wajikwamue na vikwazo vya kuporomoka kwa bei ya mahindi katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Amewahimiza kulima mazao ya biashara ikiwamo soya na ngano kuliko kutegemea mahindi pekee kama zao la chakula na biashara.

Alisema hayo juzi katika ziara yake mkoani Rukwa, huku akisisitiza kuchukua hatua kali, dhidi ya viongozi wa vyama vya ushirika wanaofanya ubadhirifu.

Bashe aliwataka viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Ufipa (UCU) kutowadai wananchama wake kulipa deni la Sh. milioni 900, ambalo lilisababishwa na baadhi ya viongozi wa chama hicho, ambao walichukua mbolea ya mkopo kwa matumizi binafsi.

Aliwaagiza viongozi wa UCU kuwa na taratibu za kumtambua wakala aliyekikopesha chama hicho, pembejeo hizo za kilimo.

Katika ziara hiyo, Bashe alibaini ubadhirifu unaofanyika katika Wilaya ya Kalambo, ambapo baadhi ya wakulima wanalazimishwa na wakopeshaji kuwalipa madebe 18, sawa na magunia matatu ya mahindi kwa mfuko mmoja wa mbolea aina ya DAP, wenye thamani ya Sh. 70,000.

"Gunia hilo moja linauzwa kwa Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) Kanda ya Sumbawanga kwa Sh. 50,000... haiwezekani mkulima awe na deni la Sh. 70,000 halafu adaiwe magunia matatu ya mahindi, sawa na Sh. 150, 000, huu ni wizi na dhuluma kwa wakulima," Bashe alionya.

# Wafugaji waelekezwa maeneo ya kulisha

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Liwale mkoa ni Lindi, Judith Nguli, amewataka wafugaji kufuata sheria na utaratibu, ikiwamo kuzingatia maeneo ambayo yametengwa kwa ajili malisho, ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kati yao na wakulima.

Alisema, mtindo wa wafugaji hao kuhama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili yao na kwenda kuishi sehemu ambayo hawajatengewa, unaweza chimbuko la migogoro kati ya makundi hayo mawili.

Nguli alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na viongozi wa wafugaji kwa lengo la kudumisha amani wilayani mwake kwa kuwa makundi hayo kila moja lina umuhimu wake kwa amani na maendeleo ya Liwale.

"Mtindo wa kuhama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili yenu na kwenda kuishi maeneo ambayo hamjatengewa, unaweza kusababisha migogoro kati yenu na wakulima, hivyo acheni mtindo huo," alisema Nguli.

Alisema, kinachotakiwa ni wafugaji na wakulima kuendelea kuimarisha amani na utulivu miongoni mwao wakati serikali ikiweka mikakati ya kuhakikisha inaboresha huduma mbalimbali ikiwamo ujenzi wa mabwawa ya maji.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliwataka viongozi wa vijiji ambavyo vina wafugaji wasitoe vibali kwa wafugaji wapya, badala yake washughulikie kero ambazo zinaweza kuleta kusababisha wakulima na wafugaji wakahasimiana.

"Kinachotakiwa ni viongozi wa vijijini kuangalia kama kuna changamoto miongoni mwa wakulima na wafuagaji katika maeneo yao wazitafutie ufumbuzi ili makundi yote yaendelee kuishi kwa amani," alisema.

Ofisa Mifugo wa wilaya hiyo, Bernard Kivamba alisema, Liwale ina ng'ombe 30, 689, mbuzi 11, 797 na kondoo 2, 462, akifafanua kuwa Kijiji cha Kimambi ndicho kinachoongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi zaidi.

Kijiji cha Kimambi kina ng'ombe 14,000 kati ya hao 30, 689, na sasa serikali inatarajia kujenga bwawa la kunywesha maji mifugo mingine lenye thamani ya Sh. milioni 480," alisema Kivamba.

Ofisa Mifugo huyo, alifafanua kuwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022, serikali imetenga Sh. milioni 480 ambazo zitatumika kujenga bwawa hilo la kunyweshea mifugo katika Kijiji cha Kimambi.

Aidha, alisema, ofisi yake imekuwa ikijitahidi kuhakikisha Liwale haina migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kushirikisha makundi hayo kila linapotaka kutokea jambo linaloweza kusababisha uhasama.

Kiongozi wa wafugaji wilayani humo, Lugora Uporo, ameahidi kushirikiana na serikali ya wilaya hiyo kuwa atahamasisha wenzake kutokuwa chanzo cha migogoro kati yao na wakulima.

"Tutaendelea kushirikiana wote kama Watanzania, ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anaishi kwa amani na utulivu na kufanya shughuli zake za maendeleo ikiwamo kilimo na ufugaji,"




Maofisa wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Meneja Masoko na Mawasiliano Grace Majige (kulia) na Meneja wa Tawi la TCB Mpanda, Julius Mlanga (wa pili kulia), wakikabidhi sehemu ya mabati bando 15 yenye thamani ya 5.4m/- kwa Ofisa Elimu wa Mkoa wa Katavi, Dk. Elipidius Baganda (wa pili kushoto), yaliyotolewa msaada na benki hiyo kwa ajili ya kupaua madarasa mawili ya Shule ya Msingi Katavi, Manispaa ya Mpanda mapema wiki hii. Kushoto ni Mstahiki Meya wa Mpanda, Haidari Sumri na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Wailes Kibona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SGA yaunga mkono upimaji wa VVU

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA imeanzisha mpango wa upimaji wa virusi vya UKIMWI mahali pa kazi kwa wafanyakazi, hafla iliyozinduliwa katika makao makuu ya kampuni hiyo hivi karibuni.

Uzinduzi huo uliendeshwa na maofisa kutoka Chama cha Waajiri nchini (ATE), PSI Tanzania, Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) pamoja na maofisa kutoka Wizara ya Afya, ambapo uongozi wa kampuni hiyo ulipewa vifaa ambavyo wafanyakazi watapata fursa ya kujipima kwa hiari.

Uongozi wa kampuni hiyo unatarajiwa kuhifadhi vifaa hivyo vinavyotarajiwa kutatoa mwamko kwa waajiriwa kujipima wenyewe wawapo majumbani mwao ili kujua hali zao kiafya kuhusiana na masuala ya VVU na UKIMWI kwa ujumla.

Akikabidhi vifaa hivyo, mwakilishi wa ATE katika hafla hiyo Hellen Mkwizu, alisema kuwa ATE inakusudia kuwezesha waajiri kujali afya za wafanyakazi wao kwa kupima hali zao kiafya ili waweze kujitunza pale wanapobaini wako salama au wachukue zinazostahili watakapojijua wameathirika.

Alitoa rai kwa waajiri wengine kuiga mfano wa SGA utakaowawezesha wafanyakazi wao kujua hali zao na kuyalinda maisha yao.

"Lengo la serikali kupitia Wizara ya Afya ni kufikia takwimu za 95:95:95, ambayo ni asilimia 95 ya kubaini walioambukizwa VVU, asilimia ya waliogundulika kuwa na VVU kupata matibabu na asilimia 95 ya walioathirika kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs)," alisema.

Aliongeza kuwa ni matumaini yake kuwa mpango huo ulioanzishwa na SGA, utakuwa wa manufaa makubwa kwa wafanyakazi wake.

Mkurugenzi wa PSI Tanzania, Ajuae Hassan, aliishukuru SGA kwa kuchukua hatua ya upimaji mahali pa kazi na kuwa mwajiri wa mfano katika mpango wa kupima maeneo ya kazi.

"Kampuni ya ulinzi ya SGA imethibitisha kuwa ni kampuni ya mfano inayoongoza si kama mwajiri mkubwa hapa nchini bali pia kwa kujali afya za wafanyakazi wake na mfano hai ni kukubali kuzindua mpango huu," alisifu.

Kampuni ya ulinzi ya SGA imeajiri zaidi ya wafanyakazi 6,000 kupitia mtandao wake ulioenea nchi nzima. Kampuni hiyo ya ulinzi ilianza shughuli zake nchini mwaka 1984, wakati huo ikijulikana kama Group Four Security.

Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, Eric Sambu, aliwakaribisha washirika katika mpango huo ambayo kampuni yao ilipata fursa ya kuandaa uzinduzi wake.

"Siri kubwa ya mafanikio yetu inatokana na uongozi wa kampuni kujali ustawi wa wafanyakazi wetu ikiwamo kujali afya zao wawapo kazini, kupitia mpango huu, kila mfanyakazi atapata fursa ya kujua hali yake ya afya kwa na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa matokeo atakayopata baada ya kujipima," alisema.

Meneja wa Afya na Usalama wa SGA, Dickson Webi, alisema afya njema na usalama wa kutosha kwa wafanyakazi vimeisaidia kampuni hiyo kufikia malengo yake ya mafanikio inayojiwekea.

# Tanzania kuendelea kunufaika na WIPO

**Na Felix Andrew**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umesema Tanzania itaendelea kunufaika na miradi mbalimbali ya Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO).

Hayo yalibainishwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, katika mkutano mkuu wa mwaka wa nchi wanachama wa WIPO ulioanza Oktoba 4, mwaka huu na utahitimishwa leo jijini Geneva, Uswisi.

Katika hotuba yake, Nyaisa alibainisha miradi ya miliki bunifu ambayo Tanzania imenufaika ikiwamo kujengea uwezo makundi mbalimbali ili kutumia miliki bunifu kwa maendeleo ya nchi .

"Mpaka sasa BRELA imeweka mfumo wa kushughulikia maombi ya hataza na alama za biashara (IPAS), mapitio ya sheria za miliki bunifu pamoja na vitabu na ufundishaji wa sehemu ya Shahada ya Uzamili ya Miliki Bunifu inayotolewa na Chuo kikuu cha Dar es Salaam," alisema.

Aliongeza kuwa, hivi karibuni WIPO na Mahakama ya Tanzania walisaini mkataba wa makubaliano kwa nia ya kuimarisha mfumo wa mahakama na huduma za miliki bunifu na ulinzi nchini. Utekelezaji wa makubaliano hayo utasaidia kushughulikia changamoto za kisheria zinazohusiana na uamuzi wa miliki bunifu unaokabili mfumo wa Mahakama nchini.

Mkutano huo utapitia na kujadili shughuli mbalimbali na kupitisha bajeti ya WIPO. Tanzania imekuwa mwanachama wa WIPO tangu mwaka 1983.

Akizungumza wakati wa kutia saini makubaliano hayo mapema mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa WIPO, Daren Tang, alikaririwa kuipongeza Tanzania na kueleza kuwa utafiti uliofanywa na jarida la kimataifa linalopima nchi mbalimbali katika masuala ya uvumbuzi katika utafiti wake ilieleza kuwa mwaka jana Tanzania ilishika nafasi ya kwanza kati ya nchi 16 zenye kipato cha chini (kwa wakati huo ) na nafasi ya nne kati ya nchi 26 za kusini mwa jangwa la Sahara.

Tang alizitaja sababu za Tanzania kufanya vizuri kuwa ni uwepo wa miundombinu mizuri ya ubunifu, mazingira mazuri ya kimawasiliano kati ya Tanzania na mataifa mengine na ongezeko la viwanda.

Hafla ya kusainiwa kwa mkataba huo ilifanyika kwa njia ya mtandao na kuhudhuriwa na viongozi wa Mahakama ya Tanzania akiwamo Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Biashara,

Stephen Magoiga ambaye alitoa ujumbe wa Mahakama kwa niaba ya Jaji Mkuu pamoja na viongozi wengine wa juu wa Mahakama. Viongozi wa WIPO na Balozi wa Tanzania nchini Uswisi, Maimuna Tarishi, aliyewakilisha Tanzania nchini humo pia alihudhuria hafla hiyo.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Innocent Rwetabura, akizungumza na watoa huduma kwa wateja wa kampuni hiyo, kabla ya kujibu na kutatua maswali ya wateja katika kituo cha kisasa cha huduma kwa wateja, kama sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja 2021, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango wa NIT wajikita kulenga mipango ya taifa

**Na Prosper Makene**

CHUO Cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT) kimeandaa mpango mkakati wa nne ambao utatekelezwa kwa miaka mitano ukilenga mipango ya taifa

Mkuu wa NIT, Prof. Profesa Zacharia Mganilwa alisema mpango huo utaanza kutekelezwa 2021/22 mpaka 2025/26. Alikuwa akizungumza wakati akiwasilisha mpango mkakati huo kwa washiriki wa semina ya wadau iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

"Mpango huo wa miaka mitano umetengenezwa kulingana na mipango mbalimbali ya kitaifa ikiwamo mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22."

Aliongeza: "Mpango mkakati huu umetengenezwa kutokana na mahitaji muhimu yaliyomo katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania (TDV 2025), Mpango wa Tatu wa Kitaifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22- 2025/26, Ilani ya chama tawala 2020, Sera ya Kitaifa ya Usafirishaji 2003, Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi 2016/17 - 2025/26 na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2016/17 - 2020/21 miongozo mingine iliyotumika ni Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango Mkakati wa Chuo uliotekelezwa kwa Miaka Mitano iliyopita yaani 2016/17 - 2020/21.

Prof. Mganilwa alisema kutokana na mapitio ya utendaji kazi uliofanywa katika mpango mkakati wa tatu ambao nao ulikuwa wa miaka mitano, wadau walipendekeza uanzishaji wa kituo cha ubora katika uendeshaji wa mafunzo ya anga, uanzishwaji wa mafunzo ya reli na teknolojia ya usafirishaji, uanzishwaji wa mafunzo ya usafiri wa majini na Kituo cha Ubora kwa Usalama barabarani, kuanzishwa kwa Shule ya Ujenzi wa meli na Teknolojia.

"Maswala mengine yaliyopendekezwa na wadau ni chuo kuwekeza katika miundombinu ya kufundishia na vifaa ikiwa ni pamoja na kujenga hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, warsha na maabara," alisema.

Aliyataja mambo mengine muhimu ambayo yamezingatiwa na mpango mkakati mpya ni kuimarisha ubora wa ufundishaji, utafiti, huduma za maktaba na teknolojia ya habari na mawasiliano, kuimarisha mifumo ya kisheria ya taasisi pamoja na kuimarisha uzalishaji wa mapato ya ndani.

"Mpango huu uliandaliwa kwa njia shirikishi ikiwa ni pamoja na kupokea maoni mbali mbali kutoka kwa wadau tukiwa na dhamira kuu ya kuwa na mpango bora kabisa wa maendeleo wa nne kwa mwaka 2021/22 - 2025/26," alisema, na kuongeza kuwa katika mpango wa tatu (2016 / 17-2020 / 21), Taasisi yao ilipata mafanikio na changamoto kadhaa hususani wakati wa utekelezaji.

"Mbali na hayo, Taasisi itaendelea kuongeza Programu za Mafunzo, Kuongeza udahili wa wanafunzi, upanuzi wa miundombinu na vifaa vya mafunzo, uanzishwaji wa Kituo cha Umahili cha Nishati (CoE), uanzishwaji wa kituo cha ujasiriamali na Biashara (NITEBIC) na uboreshaji wa mapato ya ndani," alisema.

Alisisitiza kuwa chuo hivi sasa kimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuboresha kituo cha umahiri cha anga na teknolojia ambacho kinadhaminiwa na Benki ya Dunia na uboreshwaji wa kituo cha umahiri cha usalama barabarani kinachofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Alisema kuwa mapato ya ndani ya chuo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 10.38 kwa mwaka 2016/17 hadi Sh. bilioni 17.63 mwaka 2020/21 likiwa ni ongezeko la asilimia 110.

## Benki ya Exim yaahidi kuboresha huduma

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Benki ya Exim na Watanzania kwa ujumla, wamehakikishiwa kuboreshewa huduma zaidi.

Ahadi hiyo imetolewa wakati Exim Tanzania ikiungana na watoa huduma ulimwenguni kusherehekea wiki ya huduma kwa wateja huku ikiahidi kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake ili kuongeza ustawi wao sambamba na kuongeza huduma zenye ubunifu zaidi kwenye soko la huduma za kifedha.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni, "Nguvu ya Huduma," ambayo inaonyesha umuhimu wa huduma kwa wateja na pamoja na watoa huduma katika kusaidia wateja kila siku.

Akitoa salamu za heri kwa wateja na wafanyakazi wa benki hiyo jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Jaffari Matundu, alisema kuna haja ya kulinda wateja kwa bidii na kuleta kwenye soko bidhaa za ubunifu ambazo zitasaidia kuinadi benki hiyo kama chapa yenye nguvu.

"Wiki ya Huduma kwa Wateja imetoa tena nafasi nzuri kwa benki kusherehekea jukumu muhimu ambalo tumekuwa kukilifanya kila siku yaani kuwahudumia wateja wetu na kuonyesha umuhimu wa ushirikiano baina yetu kama uongozi, wafanyakazi pamoja na wateja wetu," alisema. Kwa upande wake Ofisa Mkuu Idara ya Fedha, Shani Kinswaga, alipongeza wafanyakazi wote wa benki hiyo akisema utoaji bora wa huduma ni kiungo muhimu katika kuhakikisha wateja hao wanaridhika huku akiwataja wafanyakazi hao kama mashujaa muhimu ambao wamekuwa wakihakikisha wateja wanaridhika kupitia huduma bora wanazozitoa.


"Zaidi pia ningependa tuendelee kuzingatia na kujitolea katika kutoa huduma bora kwa wateja wetu ambao wameendelea kuwa waaminifu kwetu pia." Alisema Kinswaga wakati akihimiza timu ya wafanyakazi hao kujisikia fahari kwa michango yao.

Katika tukio hilo, ilishuhudiwa wafanyakazi hao wakihudumiwa kifungua kinywa na Ofisa Mtendaji Mkuu Bw Jaffari Matundu sambamba na kujadili pamoja maswala muhimu ikiwemo namna bora ya uboreshaji wa huduma sambamba na kujadili fursa zinazopatikana kupitia ukuaji wa biashara.

Huku akisisitiza kuwa kila siku ni siku ya huduma kwa wateja katika benki hiyo, Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Frank Matoro, alisema benki imeendelea kujitolea kutoa kiwango cha huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa wateja wake na wadau bila kujali hali zao au wapi walipo kote nchini.

"Kama sehemu ya hatua za kurejesha fadhila na uaminifu wa wateja wetu, tumepanga shughuli kadhaa za kipekee na maalum kuwathamini wateja. Baadhi ya shughuli ni pamoja na kutembelea wateja kwa kushtukiza na kuwazawadia kama njia ya kuwashukuru kwa kuwa waaminifu kwetu.," alisema

"Kuridhika kwa wateja ndiko kunatufanya tuendelee… bila wateja wetu sisi sio chochote. Kaulimbiu ya kimataifa ni 'Nguvu ya Huduma "lakini katika benki ya Exim tulienda mbali zaidi na kwa kuwa tunajivunia kuwahudumia wateja wetu, kwetu sisi kaulimbiu ni' Fahari Kukuhudumia," lisema.




Ukurasa 14

Nyama imepanda bei sasa tufanye hivi



**MSALATO YAZALIWA UPYA**

**Mkataba ujenzi Uwanja Ndege wa Kimataifa ulivyofumua tabasamu**

Ukurasa 14

BUFE
IJUMAA OKTOBA 8, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Wataalamu walia bajeti ya kijinsia msukumo uanze ngazi ya mtaani

**Na Christina Mwakangale**

ELIMU kuhusu bajeti yenye mrengo wa kijinsia, ni miongoni mwa mambo Watanzania wanahitaji, kuanzia ngazi ya familia, kaya, kata, mtaa, kijiji, jimbo hadi ngazi ya serikali kuu.

Bajeti yenye mrengo wa kijinsia inayotatua matatizo ikiwamo ukosefu wa usawa na haki ya uchumi, inatajwa kuwa na nafasi ya kuhakikisha rasilimali zote zinawanufaisha wanawake na wanaume bila ya ubaguzi.

Deogratius Temba, mwezeshaji wa masuala ya kijinsia anaelezea namna dhana tofauti kwenye jamii zimezoeleka na kurithiwa, hata kusababisha vikwazo vya maendeleo kijamii, bila ya wahusika kubaini ni tatizo.

Mtaalamu Temba anawasilisha katika mafunzo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kwa madiwani, watendaji na wenyeviti wa serikali za mitaa, kuhusu bajeti yenye mrengo wa kijinsia, anasema inalenga kuleta usawa wa kijinsia katika umilikishaji ardhi na rasilimali nyingine.

"Bajeti yenye mrengo wa kijinsia ni nyenzo inayolenga kupenyeza au kuingiza mtazamo wa kijinsia katika mchakato wa kupanga bajeti na katika mgawanyo wa rasilimali.

"Bajeti hutoa mamlaka kwa watendaji wa umma kukusanya na kutumia mapato ya serikali. Bajeti ni kioo cha kijamii juu ya sera za serikali, inatakiwa kuwa shirikishi iwezekanavyo," anasema Deogratius.

Anasema ni bajeti iliyo na usawa pande zote kazi kwa kila mtu, wanawake, wanaume, wasichana na wavulana ikitoa mgawanyo sawa wa rasilimali na uchangia fursa sawa kwa wote, ikizingatia mahitaji muhimu ya kila kundi kutokana na tofauti zao kimajukumu na kijinsia.

"Nini kinatoa uhalali wa kuzungumzia au kushawishi kuhusu bajeti yenye mrengo wa kijinsia. Inatokana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, mikataba ya kikanda na kimataifa," anasema Deogratius.

Temba anagusa mikataba hiyo na uhusiano wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia, kwamba Mkataba wa Umoja wa Afrika (AU) wa Haki za Binadamu na Wanawake 2003, inajumuisha Mkataba wa Jumyuiya ya Maendeleo ya Afrika (SADC), Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Afrija Mashariki na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu 1948.

Anaitaja mikataba mingine ni Azimio la Mpango Kazi wa Beijing, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mkataba wa Kutokomeza aina zote za dhuluma na ukatili dhidi ya Wanawake 1979, pamoja na Ajenda ya kuelekea mwaka 2063 uitwao 'Africa we Want'.

**BAJETI YA KIJINSIA**

Temba anasema, bajeti yenye mrengo kijinsia inaigusa jamii moja kwa moja kulingana na eneo husika, kwa kuchambua bajeti ya mwaka uliopita, ili kubaini mapungufu yake kijinsia.

Anasema ushiriki wa wananchi na viongozi kwenye vikao husika, unasaidia kubaini mapungufu ya bajeti na kuonyesha vipaumbele vinavyohitajika.

Temba anasema mahitaji yenye mtazamo wa kijinsia yanagusa upatikanaji huduma muhimu kijamii, ikiwamo majisafi na salama, elimu na shughuli za kiuchumi.

Anabainisha kupatikana majisafi na salama karibu na makazi ndani ya mita 400 au 300 kama ilivyoelekezwa kwenye sera husika, inakuwa ni ulinzi na usalama wa wanawake na watoto, ambao ndio watafuta maji majumbani.



Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala mkoani Shinyanga, Neema Katengesya, alipofunga mafunzo ya Bajeti kwa Mtazamo wa Kijinsia, kwa watendaji wa vijiji na kata za Shilela na Lunguya. **PICHA: MTANDAO.**

"Hili litaondoa kabisa tatizo la ndoa na mimba za ututoni, zinazosababishwa na ukosefu wa maji, usimamizi wa pamoja wa maji na ushiriki wa wanawake kwenye maamuzi ya matumizi ya rasilimali maji ni muhimu.

"Ushiriki wa wanawake katika vyombo vya maamuzi vya maji kama jumuiya za watumia maji na hata kwenye elimu, mfano kuwapo matundu ya vyoo kwa kuzingatia uwiano kama inavyoelezwa katika sera, kwa wasichana ni 1:20 na wavulana 1:25," anasema.

Anaeleza kwamba upatikanaji wa majisafi na salama yanayotiririka ndani ya vyoo, chumba cha kujisitiri kwa wasichana wakati wa hedhi nayo ina umuhimu stahiki.

Mwezeshaji mafunzo huyo anataja orodha ya mahitaji kijinsia ambayo yakizingatiwa yataongeza kiwango cha ushiriki wa wasichana shuleni na kupunguza utoro wa kila mwezi, inajumuisha kuwapo chombo cha kuhifadhi au kuharibu taka mbichi hasa za taulo za kike, pia mabweni ya wasichana.

Diwani wa Viti Maalumu kutoka Kata ya Saranga jijini Dar es Salaam, Liberatha Samson, anatoa ushuhuda mahali pake, kwamba wataanza kuchangishana fedha viongozi wa kata hiyo kufanikisha huduma hiyo, huku wakiandaa andiko kwa Halmashauri ya Ubungo, kutenga bajeti maalum kwa kasoro hiyo.

Liberatha anasema mafunzo yametoa mwanga kwa viongozi wa mtaa kuanza kutatua matatizo ya wananchi wenyewe, kwa kuweka mikakati, badala ya kusuibiri bajeti kuu ya serikali.

"Mimi nipo kwenye kamati za huduma za jamii tunaona changamoto nyingi shuleni, hasa zikiwakumba wasichana shuleni kutokana na idadi ndogo ya vyoo, maji, kukosa taulo za kike. Sasa kuanzia Oktoba, tutatoa taulo za kike na baadaye kujadili kutengwa bajeti maalumu kutoka halmashauri," anasema Liberatha.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Shakila Mayumana, anasema wanaratibu mafunzo kwa kushirikiana na Asasi ya tab COADY International, anasema utendaji mzuri wa kiongozi ni ule unaoacha alama katika jamii, katika eneo hilo kila haki ya kijinsia.

**Soma makala zaidi uk. 12**

UCHUMI

# Elimu duni ya bajeti inavyokwamisha familia katika tope la umasikini hawajui pa kutoka

- Mchungaji asimulia alivyokuwa kizani
- Mvuragano nyumbani una nafasi yake
- Kinababa: Nasi 'tunapigwa' kodi ya meza

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KUYUMBA uchumi ni miongoni mwa sababu ya migogoro kuanzia ngazi ya familia na wakati mwingine kuchangia uwapo wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii.

Inaelezwa migogoro husababishwa na kuyumba kwa uchumi katika ngazi ya familia, mara nyingi inachangiwa na kutokuwepo bajeti inayoainisha kipato na matumizi ya familia husika.

Mtaalamu wa upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia kutoka Shirika lisilokuwa la kiserikali la ELIMISHA, Festo Sikagonamo, anasema ili kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye ngazi ya familia, ni muhimu wanandoa wakapanga bajeti ya familia yao kwa pamoja yenye mrengo wa kijinsia.

Anasema bajeti ya aina hiyo, inaisaidia familia kuwa na furaka kwa sababu mke na mume wakishirikiana kupanga bajeti watafanikiwa kutekeleza majukumu yao kwa pamoja na kuepukana na msongo wa mawazo.

Aidha, anasema kwa kufanya hivyo wanafamilia wataepuka baadhi ya matatizo kama vile ugomvi, kutoaminiana na vipigo ambavyo vimekuwa na madhara makubwa ikiwemo vifo.

Baadhi ya migogoro inayotokea kwa wanandoa chanzo kikubwa huwa kuyumba kiuchumi, wanafamilia huishi kwa kuviziana na huishia kwenye ukatili.

Mwanamume hufikiri fedha za matumizi anazoziacha nyumbani, huenda mke wake anatumia vibaya, wakati huo mwanamke naye hufikiri mume anapata kipato kikubwa, lakini hakifiki nyumbani kwa kuwa hawajatengeneza bajeti ya pamoja na hakuna utaratibu wa kupanga kwa siku, wiki na mwezi.

Sikagonamo anafafanua kuwa bajeti inaweza kuwa msaada wa kukabiliana na ukatili wa kijinsia na kuokoa maisha ya wanandoa kutokana na msongo wa mawazo, pia kuleta furaha ya maisha.



Mtaalamu wa bajeti kutoka shirika la Elimisha mkoani Mbeya, Festo Sikagonamo, akitoa elimu juu ya upangaji bajeti, katika ngazi ya familia, kwa vikundi mbalimbali vya wanawake (hawapo pichani).

**FAIDA YA BAJETI**

Kwa mujibu wa Sikagonamo, miongoni mwa faida ya upangaji bajeti yenye mrengo wa kijinsia ni kuepusha migogoro ya kugombania mali kwa madai kuwa mume au mke wanaingia kwenye ugomvi, kwa sababu wanategemea mali hizo kuendesha maisha badala ya kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Anasema, udadisi walioufanya ni kwamba asilimia 75 ya makundi ya wanawake na vijana hawana elimu ya upangaji bajeti, hali inayokwamisha jitihada zao kutimiza malengo ya kujikwamua kiuchumi.

Pia, kuna kuna tatizo lingine la wanawake kukosa elimu ya kupanga bajeti, jambo linalosababisha fedha wanazopewa kama mtaji wa biashara, kushindwa kuwasaidia na wanarudi kuwa tegemezi na mtumwa kwa kuwa haruhusiwi kuhoji kipato cha mumewe.

"Uchumi ni miongoni mwa eneo linalochangia ukatili wa kijinsia kutokana na ukosefu wa elimu ya upangaji bajeti ndani ya familia, kwa kiasi kikubwa wanaume ndio huwakatili wake zao," anasema Sikagonamo.

Anaendelea: "...hususani wasiokuwa na vipato kwa maana ni mama wa nyumbani ili kukabiliana na vitendo hivyo elimu ya upangaji yenye mlengo wa kijinsia inahitajika."

**SIMULIZI ZA USHUHUDA**

Mkurugenzi huyo anaweka takwimu za kijinsia ni kwamba kati ya wanawake 10, saba wameshafanyiwa ukatili wa kiuchumi, pia vipigo.

Debora Mwanyanje, ni mtaalamu wa jinsia kutoka shirika Elomisha, anatoa ushuhuda wa ndoa nyingi zinaharibika kutokana na ukatili wa kiuchumi, mume anaposhindwa kuihudumia familia na kumuachia jukumu mke peke yake na huishia madhara mabaya ya kisaikolojia, ikiwamo mlalamikaji ama anajidhuru au kudhurika.

Kwa mujibu wa Debora, kujidhuru kwingi ni maudhui ya msongo wa mawazo, huku kukiwapo kinamama wengi wanaolazimika kuingia lindi la madeni, ili kufanikisha mradi anaokusuidia kukidhi mahitaji ya familia yake.

Regina Sanga Mkazi wa Ilolo jijini Mbeya, anayejishughulisha na kilimo cha mboga, anasema amekuwa msaada mkubwa kwa familia yake, kwani licha ya mume wake kufariki dunia miaka kadhaa iliyopita, amejitahidi kusomesha watoto na sasa wanajitegemea kwa vipato.

Anasema, maisha yake huenda yangekuwa mazuri zaidi endapo angekuwa na elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia, kwani angetumia vyema fedha anazozipata kwenye biashara yake ya kuuza mboga.

**KINABABA WAFUNGUKA**

Baadhi ya wanaume wamelalamikia wake zao kutokuwa na nidhamu ya fedha wanazoachiwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani wakidai hupeleka kwenye vikoba na upatu.

Miongoni mwao, anasema kila siku anamuachia Sh. 5,000 kwa siku, lakini haandai chakula kinachoendana na hela hiyo na wamebaini wake wana matumizi mengine na fedha hizo, jambo ambalo ni kinyume na makubaliano.

Matokeo yao hayo, ni kuanza kuona ukatili kwa watoto wasiopewa chakula sahihi, kinachozingatia vigezo vya kiafya.

Ulimbakisya Mbuto, Mchungaji wa Kanisa la Moraviani Ushirika, Tukuyu, Mbeya anasema hakuwahi kukaa meza moja pamoja na mkewe, kutengeneza bajeti, badala yake alimtegemea mke kuendesha familia.

Anafafanua, pia hakuwahi kumpa mkewe hela ya mtaji kwa ajili ya biashara na kwamba, laiti angepata elimu ya upangaji bajeti mapema, huenda angepiga hatua zaidi za maendeleo.

KUTOKA SERIKALINI

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Godfrey Kingamkono, anasema katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2020 hadi Juni 2021, halmashauri yao imetoa mikopo kwa vikundi 70, jumla ya fedha Sh. milioni 420.

Anasema vikundi vilivyonufaika ni vya wanawake 28 vimepata Sh. 168, wakiwamo wafanyabiashara na wanaoanza kujishughulisha kupitia fedha hizo.

Vilevile, vikundi vya vijana 26 kupatiwa shilingi 168 na vikundi vya wenye ulemavu 16 vikipatiwa Sh. 84.

Mkoa wa Mbeya kupitia Kamati yake ya Ushauri katika mwaka wa fedha 2020/2021, kwa Wilaya ya Kyela ilipanga kutumia fedha Sh. milioni 252 kwa kuvinufaisha vikundi 26, wanawake vikundi 10, vijana vikundi 10 na watu wenye ulemavu vikundi sita.

Katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, jumla ya vikundi 150 vya wanawake vimetengewa fedha kiasi cha Sh. milioni 422 na fedha zote tayari zimeshatolewa kwa vikundi hivyo.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, kuna jumla ya vikundi vya wanawake 17 vimenufaika na mkopo wenye thamani ya shilingi milioni 334.


Kwa Mujibu wa Ofisa ya Maendeleo ya jamii, Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile, hadi kufikia Disemba 2020 jumla ya vikundi 94 vya wanawake vimepatiwa mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya ndani kiasi cha Sh. milioni 571.



Baadhi wa wanawake jijini Mbeya, wakiendelea na shughuli za uzalishaji mali, ikiwa ni njia mojawapo ya kujikwamua kichumi. **PICHA ZOTE: GRACE MWAKALINGA**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Nyama imepanda bei sasa tufanye hivi






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

NYAMA ni chakula muhimu katika jamii yoyote ile duniani. Ndiyo sababu huchukuliwa kama chakula cha heshima, kutokana na kwamba katika karibu kila hafla au shajara nyama haikosekani.

Kwa miaka nenda rudi, nyama imekuwa kichocheo muhimu katika kuheshimisha wageni wafikapo ugenini, ambako watachinjiwa mnyama au hata ndege ili mradi nyama inakuwa sehemu ya chakula.

Mijini ukisikia mishikaki ujue ilianzia kwenye nyama, ingawa siku za karibuni kumekuwa na mishikaki ya samaki hata ya matunda, hali kadhalika nyama choma imekuwa maarufu mijini na hasa katika sehemu nyingi za starehe.

Katika familia nyingi, itokeapo sikukuu, nyama huwa ndicho chakula kikuu cha siku hiyo, ambapo mboga za majani husahaulika, licha ya wataalamu kushauri watu kula mboga kuliko nyama, kutokana na sababu za kiafya.

Pamoja na yote hayo, bado nyama inaendelea kushika usukani katika vyakula vyenye heshima katika jamii. Ndiyo sababu ikosekanapo, siku muhimu za sherehe huwa ni kizaazaa na watu kutafutana.

Mara nyingi, hususan katika sikukuu za baadhi ya imani nyama hupewa kipaumbele, mathalan kuna hatua ya uchinjaji na kutolewa sadaka kwa wasiojiweza. Hivyo, heshima ya nyama huendelea kudumishwa.

Nyama ikipanda bei huwa ni matatizo na malalamiko kutoka kwa walaji, ambao hujikamua angalau mara moja au mbili kwa wiki kupata kitoweo hicho.

Wafugaji hupewa heshima kutokana na kufuga wanyama ambao ndio huzalisha nyama. Hupandisha bei ya mifugo yao kutokana na sababu mbalimbali, hivyo wasio na mifugo kuumia kwa kujikamua zaidi ili kupata kitoweo hicho.

Nchini hivi sasa, hususan katika jiji la Dar es Salaam, bei ya nyama imepanda. Malalamiko yako kila kona. Bei sasa ni kati ya Sh. 8,000 na Sh. 10,000 kwa kilo moja ya chakula hicho.

Hali hiyo imesababisha kelele nyingi na kilio hapa na pale hata wananchi kuitaka serikali iingilie kati na kuweka bei elekezi kama inavyofanya kwa baadhi ya bidhaa kama vile mafuta jamii ya petroli.

Serikali nayo kupitia Bodi yaTaifa ya Nyama, inasema sababu kuu ni maendeleo ya kiuchumi; kwamba hivi sasa nchi ina viwanda 35 vya kuchakata na kusindika nyama kwa ajili ya kuuza kwa walaji.

Lakini, katika viwanda hivyo vitano, vinasindika nyama na kuiuza ughaibuni sehemu za Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali, hivyo nyama kuhitajika kwa wingi kwa ajili ya kulisha viwanda hivyo.

Matokeo yake ni kupungua kwa wachinjaji wadogo, hivyo nyama inaadimika na kulazimika kuuzwa kwa bei hiyo ya kuruka na kuishia walaji wa nyama kukosa mbadala na kubaki kugugumia kwa maumivu.

Yapo mapendekezo ambayo nimeyaunga mkono, kwamba ifike mahali serikali iingilie kati hususan katika utaratibu wa ununuzi wa nyama na kuondokana na utaratibu wa mnunuzi au mteja kulazimika kununua kwa kilo.

Hivi sasa mteja ananunua nyama kwa kipimo cha robo kilo, nusu kilo, robo tatu ya kilo au kilo moja na kuendelea.

Hali hiyo inafamnya mnunuzi akose chaguo na hivyo kulazimika kununua kiwango kinachopangwa na mwenye duka la nyama.

Kwanini sasa nyama isianze kuuzwa kwa kiasi cha pesa alicho nacho mtu, badala ya kilo, kwa maana kwamba badala ya mtu kufika bucha ni na kutaka apimiwe nyama kwa uzito, auziwe kulingana na pesa aliyo nayo.

Mathalan, aweze kununua nyama kwa Sh. 2,000 au hata Sh. 1,000 kulingana na pesa yake, badala ya kutumia vipimo vya uzito, ambavyo mara nyingi hulazimisha kipimo cha chini kuwa robo na kilo moja na kuendelea.

Ufike wakati mtu akifika buchani, atake nyama ya bei fulani na siya kilo fulani,ili kuondokana na kilio cha kilo ya nyama ya Sh. 10,000. Ikishindikana hiyo, basi Bodi ya Nyama iangalie jinsi ya kuhakikisha nyama za wanyama wengine zinaliwa ili mradi zisiwe na madhara. Mnaonaje? Alamsiki!

UCHUMI

MSALATO YAZALIWA UPYA

# Mkataba ujenzi Uwanja Ndege wa Kimataifa ulivyofumua tabasamu

- Prof. Mbarawa: Jamani Dodoma mtaji huo!
- RC, Wabunge: Tumeona, hatuna la kusema
- Bosi TANROADS: Tutasimamia kila kipengele

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

HATIMAYE serikali imetegua kitendawili kilichokuwa kikiumiza vichwa vya watu wengi kwa muda mrefu kuhusu lini utaanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato jijini Dodoma?

Majibu ya kitendawili hicho, yameteguliwa siku chache zilizopita, baada ya Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kutia saini mkataba wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.

Ni baada ya tukio hilo la kutia saini mkataba wa ujenzi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 36 (miaka mitatu), kuanzia sasa.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, anasema ujenzi wa kiwanja hicho utafanyika kwa awamu mbili, anaoufafanua:

"Awamu ya kwanza itahusisha kazi kuu mbili, ambazo ni ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege na ujenzi wa majengo ikiwamo jengo la abiria," anasema mtendaji huyo.

Mhandisi Mativila, anafafanua kuwa mkandarasi aliyepatikana kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ni kampuni ya Sinohydro Corporation Limited, Sino-Aero Construction Engineering Co. na M/s China Jiangxi International Economic and Technical Cooperation CO.Ltd kutoka China.

Mtendaji Mkuu Mativila, anaibainisha kuwa awamu ya kwanza itakapokamilika, kiwanja hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 1.5 kwa mwaka.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa (katikati), akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kati ya Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila (kushoto), na Mwakilishi wa Kampuni ya Sinohydro Corporation ya China, Shi Yong (kulia), jijini Dodoma.

**AWAMU II IKOJE?**

Mativila anamhakikishia Waziri Prof. Makame Mbarawa kuwa awamu ya pili ya mradi itatekelezwa kwa kutegemea mahitaji yatakayojitokeza ndani ya kipindi cha miaka 20, baada ya ujenzi wa awamu ya kwanza kukamilika.

Aidha, anasema mradi wa ujenzi huo unagharamiwa kwa ushirikiano kati ya serikali yaTanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika na serikali nchini itagharamia wastani wa Sh. bilioni 127, zitakazotumika kugharamia fidia kwa wakazi wanaopisha ujenzi wa mradi.

**MANUFAA YAJAYO**

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, anasema ujenzi wa kiwanja hicho utakapokamilika, utarahisisha usafirishaji watu na bidhaa kutoka na kuingia katika Jiji la Dodoma, pia kati ya Tanzania na nchi mbalimbali, hali inayokuza utalii na kuongeza fursa za ajira na kupanuka uchumi.

Mativila ambaye ni msimamizi mkuu wa mradi huo, anabainisha kuwa TANROADS itahakikisha kuwa kiwanja hiki hakikidhi viwango vya kitaalamu na kwa wakati.

Ndipo katika mjumuiko huo, anatoa wito kwa Mkandarasi na Mhandisi Msimamizi, kufanya kazi zao kwa weledi na ikamilike ndani ya muda stahiki waliopangiana.

**WAZIRI PROF. MBARAWA**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Mbarawa, akishuhudia utiaji saini huo, anaitaka TANROADS kuhakikisha inamsimamia mkandarasi ipasavyo, ili kukidhi ahadi ya kazi kumalizwa kwa viwango vilivyowekwa.

Prof. Mbarawa anasena, kukamilika ujenzi wa kiwanja hicho kutawezesha kutua ndege nyingi na za aina tofauti, akizitaja kama vile Airbus na Dreamliner.

Anasema kukamilika mradi huo kutaleta manufaa mengi kwa Jiji la Dodoma na nchi kwa ujumla, kwani mbali na kuimarisha sekta ya usafiri wa anga, utaleta muunganiko mzuri wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Prof. Mbarawa anafafanua kwamba, pia ni namna itafafanua shughuli za kiuchumi, kibiashara na kijamii kufanyika vizuri na kwa wakati.

Anatoa wito kwa viongozi na wananchi wa mkoa wa Dodoma hasa wanaoishi kando ya eneo la mradi, kuwapa ushirikiano wote wanaohusika na mradi wa ujenzi, ili kuwezesha utekelezaji hadi kukamilika kama ilivyo pangwa, akihitimisha kwa 'kuwazibua sikio' kwamba:

"Wananchi mnapaswa kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo, ikiwamo za ajira kwa kada mbalimbali na utoaji huduma, zikiwamo za mama lishe, usafiri na hoteli."

**WABUNGE NA YAO**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, anasema kitendo cha wizara hiyo kusaini mkataba wa ujenzi, kimejibu maswali mengi yaliyokuwa yakihojiwa na wananchi juu ya hatima ya ujenzi wa kiwanja hicho.

Anasema, kamati yao ipo tayari wakati wote kutoa ushirikiano katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi huo, ili ukamilike kwa wakati na kwa viwango vilivyowekwa.

"Ombi langu kwa wanaojenga mradi huu, zingatieni mkataba, kwani kabla ya serikali kutia saini mkataba huu, kulikuwa na maneno mengi kuwa haupo tena, lakini tunashukuru," anasema Mbunge Kakoso.

**RC NA WANADODOMA**

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, anasema kwamba kuanza ujenzi wa mradi huo, ni hatua kubwa sana kwa serikali kufanikisha mipango yake.

"Mheshimiwa Waziri, kukamilika kwa uwanja huu itakuwa ni hatua kubwa sana hata katika masuala ya kisiasa hasa pale tukapofika 2025," anasema Mtaka, huku akimshukuru Rais kwa kuboresha makao makuu ya nchi, ikiwamo ujenzi huo wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Antony Mavunde, anahitimisha maoni akisema ujenzi wa kiwanja hicho cha ndege, inainua furaha yao wenyeji wa jiji hilo, wakiutafsiri ni utambulisha wao Dodoma kitaifa na kimataifa.



Ndivyo ulivyo mwonekano wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kitakavyokuwa.
**PICHA ZOTE: PAUL MABEJA**



## Posta kuchangia ukuaji wa uchumi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Andrea Kundo, amesema Shirika la Posta Tanzania (TPC) limejipanga kuhakikisha linachangia ukuaji wa uchumi kwa kasi'.

Kundo alitoa kauli hiyo juzi baada ya kuzindua duka la Posta mtandaoni jijini hapa.

Alisema uwapo wa duka hilo unalenga kusogeza karibu huduma za Posta na wananchi na kuwarahisishia kufanya biashara mtandaoni kwa njia salama na zinazoaminika na kwa mfumo rahisi wa kidigitali.

"Napongeza Shirika la Posta kwa hatua hii, sasa shirika linakwenda sawia na mabadiliko ya teknolojia ambalo ni hitaji la wengi katika dunia ya sasa ya kidigitali,"alisema.

Alieleza kuwa mawasiliano kwa njia ya Posta ndiyo mawasiliano mama yaliyozaa mawasiliano yote duniani, na kusisitiza kuwa Posta inakuwa na kubadilika kufuatana na mabadiliko na mahitaji ya binadamu.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema uanzishwaji wa duka hilo ni mafanikio makubwa na ni jambo la kujivunia kwa Tanzania ambayo msingi wake ni umoja, ubunifu na mshikamano.

Awali, Kaimu Posta Masta Mkuu wa Shirika hilo, Macrice Mbodo, alisema uzinduzi wa duka hilo unabadili sura ya Posta Tanzania kutoka kuaminika kuwa Shirika linaloshughulika na usafirishaji wa barua tu na kwasasa linaloshughulika na usafirishaji wa bidhaa hivyo litakuwa kiungo muhimu kwa wafanyabiashara wa aina zote ndani na nje ya nchi.

**Awali, Kaimu Posta Masta Mkuu wa Shirika hilo, Macrice Mbodo, alisema uzinduzi wa duka hilo unabadili sura ya Posta Tanzania kutoka kuaminika kuwa Shirika linaloshughulika na usafirishaji wa barua tu na kwasasa linaloshughulika na usafirishaji wa bidhaa hivyo litakuwa kiungo muhimu kwa wafanyabiashara wa aina zote ndani na nje ya nchi.**

# Halmashauri 17 kupungukiwa chakula

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema licha ya nchi kutarajiwa kujitosheleza kwa chakula kwa kiwango cha ziada, bado kuna halmashauri 17 kwenye mikoa ninane zitakuwa na upungufu wa chakula kwa mwaka 2021/22.

Waziri wa Wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yatakayofanyika kitaifa mkoani Kilimanjaro kuanzia Oktoba 10 hadi 16, mwaka huu.

Alisema hali hiyo imetokana na sababu mbalimbali ikiwamo mtawanyiko mbaya wa mvua na visumbufu vya mazao shambani vilivyojitokeza katika msimu wa 2020/21.

Akizungumza bila kuweka wazi Halmashauri hizo, Prof. Mkenda alisema serikali inaendelea kufuatilia hali ya usalama wa chakula katika halmashauri hizo ili kuhakikisha hali ya utengamano inaendelea kuwapo.

Alifafanua kuwa tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonesha kuwa hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa katika msimu wa 2020/21 na upatikanaji wake kwa mwaka 2021/22 umefikia tani milioni 18.4 ikiwa ni ongezeko la tani Milioni 1.9 sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2019/20.

"Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/22 nchini, ni tani Milioni 14.7, hivyo nchi inatarajiwa kuwa na ziada ya tani Milioni 3.6 za chakula ambapo tani milioni 1.2 ni za mazao ya nafaka na tani Milioni 2.4 ni za mazao yasiyo nafaka, kiwango hiki cha uzalishaji kitaiwezesha nchi kujitosheleza mahitaji yake ya chakula kwa uwiano wa utoshelevu wa asilimia 125,"alieleza.

Kuhusu maadhimisho hayo, Waziri huyo alisema yatazinduliwa Oktoba 10 na kufikia kilele chake Oktoba 16, 2021 katika viwanja vya shule ya msingi Pasua, Manispaa ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro.

Alisema shughuli mbalimbali zitafanyika ikiwemo maonyesho ya kazi zinazolenga kuongeza uzalishaji, tija na upatikanaji wa chakula na usindikaji wa mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Aidha alisema elimu itatolewa juu ya kuandaa vyakula mbalimbali, lishe bora, uhifadhi na usindikaji wa mazao ya chakula, mifugo na uvuvi katika ngazi ya kaya na jamii na kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya vyakula vya asili katika ngazi ya kaya na jamii.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati) na Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma wakikata utepe kuzindua ofisi za Mahakama ya Mwanzo Kibaigwa, wilayani Kongwa, mkoani Dodoma, jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remedius Mwema na (kushoto) ni Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Najma Giga. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# NEEC yatakiwa kutafiti mitaji na riba

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), limetakiwa kufanya utafiti kuhusu suala la mitaji na riba ili kusaidia kuonyesha namna mitaji inavyopatikana, athari za riba kubwa na kuimarisha uchumi wa Watanzania.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na Bodi pamoja na menejimenti ya NEEC jijini hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuonyesha njia za kuzipunguza riba kama namna ya kuwawezesha Watanzania kuimarika kiuchumi.

Aidha alisema sera ya uwezeshaji ni mtambuka na inamhusu kila mtu na sekta zote hivyo kuna umuhimu wa Baraza kuwaelewesha wananchi na kila sekta ili watambue kuwa wanalo jukumu la kuitekeleza sera hiyo.

Hata hivyo, alisema Baraza lina kazi kubwa ya kuwalea wajasiriamali wanaofanya vizuri na kutoa ajira kwa watu wengine.

Alisisitiza wajasiriamali wapewe ushauri na kuwapendekeza kupata mikopo nafuu na kusaidiwa vitendea vya kisasa ili kuongeza uzalishaji na kutoa ajira kwa wananchi wengi.

Awali, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Beng'i Issa, alisema watahakikisha mipango iliyopo inafanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwawezesha wananchi kwa kuandaa sera ya Taifa ya ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji na miradi ya kimkakati kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alisema mipango ya Baraza hilo ni kuendeleza vituo vya uwezeshaji katika ngazi ya mikoa na halmashauri, kuratibu utendaji wa jukwaa la wanawake kiuchumi katika ngazi ya mikoa na halmashauri na ujenzi wa jengo la Ofisi kwa ajili ya matumizi ya Baraza.

Prof. Lucian Msambichaka, ambaye ni mjumbe wa bodi hiyo, alimhakikishia waziri kuwa maelekezo aliyoyatoa watayatekeleza kwa wakati ili kuhakikisha wananchi wanawezeshwa kiuchumi.





# Ukosefu kituo afya watesa wananchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU saba wakazi wa Kata ya Ulenje katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamefariki dunia kwa nyakati tofati wakati wanasafirishwa kwa gari binafsi ya diwani wa kata hiyo kupelekwa katika hospitali.

Walikuwa wanasafirishwa kwa gari la diwani huyo, Mhandisi Bonface Njombe kupelekwa hospitali za Jiji la Mbeya kutokana na kata hiyo kutokuwa na kituo cha afya.

Hayo yalisemwa juzi na Diwani huyo wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, Mwanaidi Ally Khamisi, ya kutembelea Shule ya Maadilisho ya Ilambo iliyopo katika Kata hiyo.

Alisema wananchi wa kata hiyo huwa wanalazimika kwenda kupata huduma za matibabu jijini Mbeya, ambako kuna umbali wa zaidi ya Kilomita 50, na kwamba inapotokea mtu amezidiwa huwa inakuwa vigumu kuokoa maisha yake.

Mhandisi Njombe alisema Kata hiyo inazo zahanati kwenye vijiji vitatu ambazo zinatoa huduma, lakini inapotokea mgonjwa anahitaji matibabu zaidi huwa inakuwa vigumu, na kwamba ndio maana huwa wanasafiri kwenda Mbeya Mjini.

Alisema tatizo huwa linakuwa kubwa zaidi nyakati za usiku kutokana na kipindi cha mvua kutokana na barabara kuwa mbovu, hali ambayo alidai wagonjwa huwa wanaumia wakati wakisafirishwa kwenda kutibiwa.

"Mimi mwenyewe ni shuhuda, watu wangu kama saba wamefia kwenye gari yangu binafsi wakati ninapowasafirisha kuwapeleka kwenye hospitali zilizopo mjini, huwa naumia sana unamsafirisha mjamzito halafu unasikia analalamika kuwa anaumia kwa sababu ya barabara kuwa mbovu," alisema Njombe na kuongeza:

"Tunaamini kuwa tukiwa na Kituo cha afya kwenye kata yetu tutapunguza hili tatizo la watu kupoteza maisha, hivyo mimi na wananchi wangu tumeshaanza jitihada za kujenga Kituo cha afya kwa nguvu zetu na tutaomba serikali ituunge mkono."

Alisema mpaka sasa wananchi wa kata hiyo wamefyatua matofali 80,000 na kuzichoma kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya, na kwamba tayari wanalo eneo lenye ukubwa wa ekari sita kwa ajili ya mradi huo.

Nao baadhi ya wanawake wa Kata hiyo waliiomba Serikali iwasaidie kuboresha barabara ili anagalau kupunguza tatizo la kumia wakati wanasafirishwa wakidai kuwa wakati mwingine ubovu huo wa barabara ndio huwa chanzo cha kupoteza maisha.

Mmoja wa wanawake hao, Winfrida Mwakisyala, alisema wakati mwingine wanapoenda kujifungua kwenye zahanati zilizopo kwenye vijiji vyao wanaambiwa kuwa wana matatizo na hivyo kutakiwa kwenda kujifungulia kwenye hospitali kubwa.

Alisema wakati mwingine huwa wanashindwa kusafiri kwenda kwenye hospitali hizo kutokana na kutokuwa na uwezo kiuchumi wa kusafiri hali ambayo alidai huwa inasababisha madhara kwao ikiwemo vifo kwa mama wajawazito na watoto.

"Wengine huwa wanakufa kwa sababu ya kuchelewa kufika hospitalini kujifungua, lakini wengine huwa wanajifungua watoto waliokufa kutokana na barabara zetu kuwa mbovu kwahiyo watoto huwa wanaumia wakati wa kusafirishwa," alisema Winfrida.

Kutokana na adha hiyo, Naibu Waziri Mwanaidi alisema atazungumza na viongozi wa ngazi mbalimbali mkoani Mbeya kuhakikisha wanawekeza nguvu kuwaunga mkono wananchi kwenye ujenzi wa Kituo hicho.

Aliwapongeza wananchi wa Kata hiyo kwa kuamua kujenga Kituo hicho akisema wananchi hao ni mfano kwa wakazi wa maeneo mengine nchini kujitolea kujenga miundombinu ya aina hiyo.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi (kulia), akipata maelezo kuhusu kilimo cha matango kutoka kwa Shukuru Tweve ambaye ni mmoja wa wataalamu wa Shirika la Helvetas ambao ni watekelezaji wa mradi wa kuboresha mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani wa Agri-Connect katika Kata ya Inyala, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Rujewa wataka kasi mchakato wa kuwa halmashauri kamili

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WENYEVITI wa vitongoji katika Mamlaka Mji Mdogo Rujewa wilayani Mbarali, wameiomba Serikali kukamilisha mchakato wa mamlaka hiyo kuwa halmashauri kamili iweze kujitegemea katika shughuli mbalimbali na kuharakisha maendeleo kwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mwenyekiti wa Mamlaka Mji Mdogo Rujewa, Elly Kimilike, alisemai ni muda mrefu sasa wamekuwa wakiiomba Serikali iwapatie halmashauri kamili ili ijitegemee na kukusanya mapato kwa ajili ya kusogeza karibu huduma za kijamii kwa wananchi.

Aliongeza kuwa uongozi wa wilaya ungetoa taarifa mapema juu ya kusua sua kwa mchakato huo wasingekubali kukatwa posho zao.

"Tunamkumbusha Mkurugenzi kwamba inabidi atulipe fedha zetu zote tulizokatwa kwa miaka sita kila mmoja Sh 20,000 kwa ajili ya kuhakikisha kuwa tunapata halmashauri kamili katika eneo la Ubaruku wakati tukisubiri maelekezo ya serikali alisema Kilemile," alisema.

Aliongeza kuwa katika kikao hicho walitegemea kila mjumbe apate fedha zake kwa sababu wakati wanakaa na kukubaliana kupunguza fedha zao uongozi wa halmashauri haukuweka bayana kuwa suala la halmashauri halitawezekana hivyo waliomba warudishiwe fedha zao.

Diwani wa Rujewa ambaye pia ni mlezi wa Mamlaka hiyo, Jeremiah Makao, alisema suala hilo limefikishwa rasmi kwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa, kupatiwa ufumbuzi na kuwataka wenyeviti kasi na kuwasisitiza wenyeviti kuendelea kudai halmashauri kamili ili kujiletea maendeleo.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Oliver Sulle, ambaye pia Ofisa Tawala wa Halmashauri hiyo alisema suala la ukamilishaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa kuwa halmashauri kamili linatakiwa kutekelezwa kwa mujibu wa sheria hivyo lazima taratibu zifuatwe.

"Wenyeviti wa vitongoji nawaomba muwe watulivu tusilazimishe kwa sababu haya mambo yanafanyika kwa mujibu wa sheria na ukizingatia tayari Chama cha Mapinduzi nao wameongeza nguvu ili kushughulikia suala hili naamini jambo litakuwa sawa," alisema Sulle.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Lihuwi Ngonyani, alisema mchakato wa kupandisha Mji mdogo Rujewa kuwa halmashauri kamili unaendelea kufanyika lakini mchakato huo ulisimama baada ya serikali kusitisha shughuli za upanuzi wa Miji.

Hata hivyo alisema inatambua umuhimu wa kupeleka madaraka na mamlaka kwa wananchi kwa lengo la kufikisha huduma karibu na wananchi, mchakato unaendelea wanasubiri maelekezo.

## TADB yaomba ushirikiano wakulima, wafugaji wavuvi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imewaomba wadau mbalimbali wa kilimo, mifugo na uvuvi nchini kuendelea kushirikiana ili kuinua sekta hiyo kwa lengo la kuinua uchumi wa wananchi na taifa.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Benki hiyo, Frank Nyambundege, wakati wa kuadhimisha wiki ya huduma kwa wateja katika Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambapo alisema sekta hizo ni muhimu kiuchumi.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo kwenye sekta hizo pamoja na kuchangamkia mikopo inayotolewa na Benki hiyo ili wajiinuwe kiuchumi na kuchangia katika ukuaji wa pato la taifa.

"Sisi kama TADB tunayo dhamana ya kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta hizi muhimu ili ziweze kutoa mchango stahiki katika ukuaji wa uchumi wa taifa sambamba na kumwezesha mkulima, mfugaji na mvuvi mmoja mmoja kuongeza uzalishaji na kukuza kipato chake," alisema Nyabundege.

Nyabundege alisema mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Songwe na Rukwa ipo katika nafasi nzuri ya kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na hivyo kuimarisha mnyororo wa thamani ya mazao hapa nchini.

Alisema katika kuadhimisha wiki ya huduma kwa wateja wataalamu wa Benki hiyo walikaa na wateja na kuwasikiliza matatizo yanayowakabili na kwamba walijifunza vitu vingi ambavyo vitawasaidia kwenye uboreshaji wa huduma.

Alisema katika mazungumzo na wateja walibaini kuwa wananchi wana uelewa mkubwa kuhusu shughuli mbalimbali za uzalishaji lakini tatizo linalowakabili ni mitaji midogo na hivyo wanawakaribisha kupata mikopo kwenye benki hiyo.

Alisema alikutana na makundi ya wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na viongozi wa taasisi mbalimbali zinazohusiana na sekta hizo na kwamba wengi waliomba kusaidiwa kuboresha shughuli zao.

"Nimefarijika kujionea mwenyewe nini kinachofanyika na kuwasikiliza wakulima wenyewe, wamenieleza matatizo yanayowakabili na nimepata picha nzuri ya namna benki itakavyofanya kutatua matatizo hayo na niwaahidi tu wananchi kwamba sisi kama benki tutaendelea kuwa karibu nao," alisema Nyabundege.

Alisema TADB kama ilivyo kwa taasisi zingine za serikali ina jukumu la kutekeleza malengo ya Serikali yaliyosababisha kuanzishwa kwa benki hiyo na akawahakikishia wananchi kwamba benki hiyo imejipanga kuwafikia wakulima , wafugaji na wavuvi kwa wakati.



# AU yatia mkono kuzuia biashara ya binadamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHENI ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika (AU) imeweka sera ya kinga dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu na uhamaji haramu kwa lengo la kupiga vita uvunjifu wa haki za binadamu barani Afrika.

Akizungumza jana katika ufunguzi wa mkutano wa kuthibitisha sera hiyo katika Ukumbi wa Hoteli ya Madinatul Bahri huko Mbweni, Zanzibar, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema umefika wakati wa kuhakikisha uhalifu huo unapotea Afrika.

Waziri huyo alisema kuwa kwa muda mrefu barani Afrika kumekuwa na matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu kwa kusafirisha watu kwenda nje ya Afrika, jambo ambalo huwaletea madhara makubwa wanapofika ugenini.

Alisema ni jambo lisilopingika kuwa nchi nyingi za Afrika, ikiwamo Tanzania, zinaathirika vibaya kutokana na usafirishaji haramu wa binadamu licha ya kuwapo sheria ya kimataifa inayokataza uhalifu huo.

"Uhalifu huu huwaathiri na kuwakumba zaidi wanawake na watoto na kupelekwa nchi mbalimbali ikiwamo Mashariki ya Kati na hata barani Ulaya ambako hukutana na vitendo mbalimbali vya uvunjifu wa haki za binadamu, ikiwamo mauaji," alisema.

Waziri huyo alisema uthibitishwaji wa sera ya kinga ya usafirishaji haramu wa binadamu na kinga ya uhamaji haramu katika Bara la Afrika ni hatua muhimu na utasaidia katika kuondoa uhalifu huo.

Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Wahamaji (IOM) Tanzania, Qassim Sufi, alisema shirika hilo linatambua madhara ya uhalifu huo ambao kwa kiasi kikubwa husababishwa na hali ya kukosekana kwa amani na utulivu katika baadhi ya mataifa ya Afrika.

Alisema licha ya kuwapo kwa sera hizo, ipo haja kwa kila nchi mwanachama wa AU kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha raia wanalindwa, hasa wanawake na watoto.

Alisema IOM inapenda kuona haki za binadamu zinalindwa hasa kwa wahamaji kwa kuwa ni haki ya kila mwanadamu kuheshimiwa na kupewa haki zake popote duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Michezo Utamaduni, Kazi, Ajira na Uhamaji wa AU, Sabelo Mbokazi, alisema Bara la Afrika haliwezi kuwa na amani wala maendeleo ikiwa uhalifu wa kusafirisha binadamu unaendelea kuwapo.

Alisema upatikanaji wa sera za binadamu na uwapo wa sera na sheria madhubuti, utasaidia kuhakikisha raia wa Afrika wanabaki salama katika mataifa yao.

Mkurugenzi huyo alisema utekelezaji wa sera mbili zinazotarajiwa kuthibitishwa katika mkutano huo ni miongoni mwa hatua madhubuti zinazoweza kusaidia katika kutokomeza uhalifu huo barani Afrika.

Hata hivyo, alisema umefika wakati wa kuhakikisha wahalifu wote wanaohusika na uhalifu huo wanafikishwa katika vyombo vya sheria na kufunguliwa mashtaka ili kukomesha vitendo hivyo.

Mkutano huo uliolenga kuthibitisha Sera ya Kinga ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Kinga ya Uhamiaji Haramu umehudhuriwa na nchi mbalimbali za AU, zikiwamo Zambia, Algeria, Mauritania na Tanzania.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohammed, akifungua mkutano wa kuthibitisha rasimu ya sera ya kinga ya usafirishaji haramu wa binadamu na kinga ya uhamiaji haramu katika bara la Afrika, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uelewa wa nguvu ya mtoto kike wamulikwa Matukio 840 ukatili miezi 8

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAKATI dunia inaadhimisha siku ya mtoto wa kike, bado baadhi ya jamii zina uelewa mdogo na zimeshindwa kutambua umuhimu wa nguvu ya mtoto wa kike kwenye jamii.

Kauli hiyo ilitolewa jana mjini Zanzibar na Sumaiya Sadik Juma aliposoma risala kwa niaba ya watoto wezake wa kike katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa kike Duniani ambayo kilele chake ni Oktoba 11 ya kila mwaka.

Alisema wapo wanajamii wanaoendelea kuamini kuwa mtoto wa kike si sehemu ya watu muhimu na kuwa na masikitiko na kilio cha muda mrefu cha matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

"Masikitiko makubwa yanayoendelea kuzitesa na kusononesha nyoyo zetu wakati leo hii sisi tunakutana hapa na kuadhimisha siku hii, taarifa za kina zinaonesha kuwa kutoka Januari hadi Agosti mwaka huu, jumla ya matukio 838 ya udhalilishaji yameripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi Unguja na Pemba huku watoto wa kike wapatao 567, sawa na asilimia 68 wakiripotiwa kubakwa na kesi hizo zipo katika hatua mbalimbali," alisema.

Alisema ni dhahiri kuwa mtoto wa kike bado hayuko salama na anahitaji ulinzi wa kina kwa kila mmoja ili kumkinga na janga hilo ambalo miongoni mwa matukio yake ni athari za kisaikolojia na kupelekea wengine kukatisha kabisa ndoto zao za kusoma na kuwa wataalamu wabobezi nchini.

Akizungumzia kuhusu hali halisi ya vikwazo vya kisheria Zanzibar wanaozokumbana nazo watoto wa kike, alisema baadhi ya vipengele bado vinahitaji marekebisho kwa lengo la kupunguza ama kumaliza kabisa vikwazo hivyo ikiwamo matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema licha ya uwapo wa ushahidi kwa mfumo wa elektroniki katika sheria lakini bado utekelezaji wa sheria hiyo umeshindwa katika mahakama kwa madai ya kukosekana kwa vifaa ambavyo vingeweza kusaidia utekelezaji wa sheria hiyo na kurahisisha watendaji wa matukio hayo kutiwa hatiani kwa urahisi zaidi. Alibainisha kuwa baadhi ya watoto wa kike walifanyiwa unyama kwa nyakati tofauti na kuwasababishia majeraha yasiyoweza kufutika akilini mwao na kupelekea kuachana kabisa na masomo na hadi sasa wamekuwa waathirika waliobaki majumbani mwao huku wakipoteza kabisa mwelekeo wa maisha.

"Ndugu mgeni rasmi na wageni waalikwa, sisi watoto wa kike tunaamini ulinzi salama dhidi yetu ndio njia ambayo itatupelekea na kutufanya sisi kushika nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa ushiriki wa wanawake kweye nafasi hizo ni jambo lisiloepukika kwa sasa," alisema.

Alitoa wito kwa watoto wenzake kuongeza kasi ya kusoma na kutokaa kimya pale wanapokumbana na vikwazo, wakiamini kuwa kukaa kimya si suluhisho ya matatizo yao.

Akifungua kongamano hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike, Salma Saadat, alisema siku hiyo inalenga kutambua haki za wasichana na matatizo yanayowakabili ulimwenguni.

Alisema kuwa mtoto wa kike anakabiliwa na vikwazo vingi ambavyo vinachangia kwa kiasi kikubwa kuzima ndoto zake.

Alisema kuwa miongoni mwa changamoto hizo ni mifumo kandamizi katika jamii, mifumo ya kisheria ambayo sio rafiki, mitazamo hasi katika jamii, ndoa na mimba za utotoni zinazosababisha mtoto wa kike kutotimiza malengo yake.

Mwenyekiti huyo alisema vitendo vya udhalilishaji nna ukatili wa kijinsia vimekuwa vikiwaumiza watoto wa kike na kuwaathirika kisaikolojia, kimwili na kiuchumi kwa sababu hukatisha ndoto zao na kuendelea kuwa tegemezi.

## Mke wa Makamu Rais atoa mbinu kwa wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, amewataka wanawake kufanya kazi kwa moyo wa kujitolea na uwajibikaji ili kufikia mustakabali bora wa kuiongoza jamii na taifa.

Aliyasema hayo jana katika Jimbo la Ziwani, Mkoa wa Kusini Pemba alipozungumza na wanawake wa Chama cha ACT-Wazalendo.

Aliwashauri wanawake juu ya dhana ya mshikamano na kuvumiliana ili kuyafikia malengo ya uzalendo na kujiendeleza katika nyanja tofauti za kimaisha, ikiwamo elimu, biashara na kupambana na wimbi la umaskini.

Akizungumzia umuhimu wa wanawake kushika nafasi za uongozi, Zainab alisema ipo haja ya kujitokeza kupitia fursa na njia mbalimbali ikiwamo kuchukua fomu kupitia vyama vya siasa na jumuiya zinazowaunganisha ili dhamira hiyo kutekelezwa.

Zainab aliwataka wanachama waliojitokeza kuchukua kadi za uanachama na fomu za uongozi, kusimamia vyema falsafa na misingi bora ya kuwaongoza watu ikiwamo maadili mema.

"Jamii inahitaji wanawake viongozi lakini watakaoheshimu misingi ya umoja, uaminifu na watakaoendeleza mshikamano badala ya kuwagawa na kuwabagua watu kwa kuendekeza maslahi binafsi," alionya.

Mjane wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, Awena Sinani Masoud, alisema viongozi wa jumuiya, taasisi na vyama vya siasa, wakiwamo wa ACT-Wazalendo, wanao wajibu wa kuwafikia wananchi na wanachama katika ngazi zote ili kuwajengea uelewa na moyo wa kujitolea katika kufanikisha maendeleo.

Aliwataka wanawake wa chama hicho kuepuka mitafaruku na migogoro inayotokana na kutanguliza maslahi binafsi, ili kuwa walimu bora wa siasa katika taifa kwa kutekeleza dhana za umoja, ukweli na uwazi pamoja na kuendelea kulinda na kuunga mkono maridhiano ya kisiasa Zanzibar.

Mwenyekiti wa Wanawake wa ACT-Wazalendo wa Mkoa wa kichama wa Chakechake, Mpaji Abass Yussuf, aliwapongeza wanachama wapya 400 waliojiunga kupitia hafla hiyo, akisema ni ishara ya imani na azma ya kuendeleza harakati za kufikia malengo muhimu ya kuipigania na kuijenga Zanzibar mpya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

KIWANJA KINAUZWA
KIPO KISUKURU JKT
SEGEREA DAR ES SALAAM,
UKUBWA SQM 2252, KINA
HATI, BEI 60 MILIONI.
**MAWASILIANO: 0655 857523.**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SALMA KARIM ALIBHAI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya RANGE ROVER SPORT yenye namba za usajili T 999 CVU chasis namba SALWA2FE4EA336458 engine namba 0781381306DT,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa DAR/BUG/RB/466966/2021

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NA 23/2021**
**ELIBARIKI NDEKIRWA………MDAI WA KWANZA**
**HELLEN WAKUGANDA……….MDAI WA PILI**
**DHIDI YA**
**MARY KASHULIZA………………MDAIWA**

**KWA.MARY KASHULIZA**
**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba mdai amefungua madai dhidi yako,nakala ya madai hayo yanapatikana katika mahakama hii
Shauri limepangwa kutajwa mnamo trehe 25/10/2021 saa 2:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya
Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo,shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena,na maamuzi kutolewa
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 4 mwezi 10 m[illegible]

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.304/2021**

Ombi la **NURU MUSSA HURUKU** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MUSSA RAJABU HURUKU**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 15/10/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukagulia
**Tarehe 04/10/2021**

Tarehe 4/10/2021
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 84/2021**
**Katika Shauri la Mirathi ya**
**ANTHONY LUMULIKO MWINAMI………………Marehemu**
**Katika shauri la maombi ya kumteua Msimamizi yaliyoletwa na**
**UPENDO ANTHONY MWINAMI…………………Mwombaji**
**TANGAZO KWA UMMA**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 08 Mwezi wa 10 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu. Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 23 Mwezi 09 Mwaka 2021.

---

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI**
**WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.**
**NA. MG/LD/3668/3/JMD**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: BRUNO KAHANGWAN**
**S.L.P 737,MOROGORO.**
**ARDHI: KIWANJA NA. 65 KITALU "LD" MLIMANI**
**MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: BRUNO KAHANGWA**
**S.L.P 737, MOROGORO.**

Taarifa inatolewa kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO ikionekana , irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA – MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO.

VALENCY HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

**VALENCY HK**
**KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA**
**MOROGORO**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 64 YA 2021**
**YONA LUCAS MAKI ……………………….MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**STEPHEN KEBWE**
**NYABANOSI MARO KYARIGA ………….WAJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**STEPHEN KEBWE**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 26/10/2021 mbele ya mwenyekiti M.Khassim wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 30 mwezi september 2021

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**DIONIS JOACHIM LYAKURWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta yenye namba za usajili T624 DNE aina ya MASSEY FERGUSON Rangi Nyekundu yenye Chasis No. F144144,Engine No.F144144. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/483945/2021**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

EMMANUEL FELIX KIMARIO Anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya bajaji yenye no za usajili T703CWK kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Rb Namba. MOR/MOR/RB/483929/2021

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 18 OF 2021**

**In the Matter of the Late EMMANUEL LISUNGU MAKULUNI BY 1. ARTHUR L. MAKULUNI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner. Objection to the grant should be filed on or before the 27th day of OCTOBER, 2021.
Dated at MOROGORO this 4th day of OCTOBER, 2021.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER ELMADA NYAGORI ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 871 CLY – TOYOTA ALTEZZA. CHASSIS NAMBA GXE100074656. ENGINE NAMBA IG9339027. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: MKB/RB/200/2021.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA MAALUM

# Namna Rais Samia alivyotafuna mfupa mgumu bei ya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI dunia ikianza kung'atwa na ongezeko la bei ya mafuta, Rais Samia Suluhu Hassan, ameonyesha njia kwa 'kutafuna mfupa' uliokuwa ukiumiza wananchi wakati bei ya bidhaa hiyo muhimu inapopanda.

Kwa kuagiza mawaziri wa wizara zinazohusika na suala hilo pamoja na taasisi nyingine za serikali kukutana na kutafuta njia ya kutoka, Rais Samia alifanikiwa kujibu mojawapo ya maswali makubwa yaliyokuwa yakiulizwa nchini kuhusu 'kwa nini bei za mafuta Tanzania wakati mwingine huwa kubwa kuliko hata katika nchi zisizo na bandari?'



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA : MTANDAO**

Matokeo ya hatua hiyo ya Rais ni kwamba sasa baadhi ya tozo zilizokuwa zikiwekwa katika bidhaa hiyo zimeondolewa na kusababisha bei kutopanda kwa kiwango ambacho kwa kawaida kingepanda.

Hatua hiyo moja ya Rais Samia imesababisha kushuka kwa bei ya mafuta kwa kiwango ambacho kinaonekana. Kwa mfano, kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Mafuta (EWURA), Godfrey Chibulunje, bei ya mafuta ilipaswa kuongezeka kwa kiasi cha Sh. 145 jijini Dar es Salaam mwezi huu, lakini sasa imepanda kwa Sh. 12 tu.

Lakini ni nini hasa kimemfanya Rais Samia kuingilia kati na kufikia uamuzi huo? Waziri wa Nishati, January Makamba, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dodoma wiki hii kuwa ni uamuzi wa kihistoria.

Tangu kuibuka kwa janga la ugonjwa wa UVIKO-19 takriban miaka mitatu iliyopita, bei ya mafuta kwa ujumla katika Soko la Dunia ilishuka kwa kiwango kikubwa. Kuna nyakati bei ya pipa moja la mafuta ilifika kiwango cha chini kabisa cha dola 10. Hali hiyo ilisababishwa na kusimama kwa shughuli za usafiri na uzalishaji wakati wa janga hilo.

Kutokana na kuanza kupungua kwa athari mbaya za ugonjwa wa UVIKO-19 na hasa baada ya kupatikana kwa chanjo za ugonjwa huo, hali ya watu kusafiri na uzalishaji imeanza kuongezeka na hivyo kuongezeka pia mahitaji ya mafuta. Katika uchumi wa soko, ukuaji wa mahitaji ni mojawapo ya sababu kubwa ya ongezeko la bei.

Rais Samia alianza urais wake Machi 19, mwaka huu na tangu aingie madarakani, bei ya mafuta imepanda juu kwa takribani mara tatu; Aprili, Julai na Septemba. Muda wake wa kuingia madarakani umegongana na ongezeko kubwa la bei ya mafuta ambapo sasa imefika wastani wa dola za marekani 80 kwa pipa - kiwango cha juu zaidi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Kufikia mwishoni mwa Septemba mwaka huu, kuna maeneo bei ya mafuta ya petroli ilifika kiasi cha Sh. 2,600, kiwango ambacho hakijawahi kuonekana katika kipindi cha walau muongo mmoja uliopita.

Wasaidizi wa Rais Samia wameiambia Nipashe kwamba tangu aingie madarakani, Rais amekuwa mfuatiliaji sana kila wakati kunapoibuka habari ya kupanda kwa bei yoyote ya kitu kinachotumiwa na wananchi wa kawaida.

"Tangu siku yake ya kwanza madarakani, Rais Samia amekuwa mtu wa kufuatilia sana haya mambo ya kupanda bei kwa vitu. Kitu kikipanda bei au akisikia malalamiko ya wananchi, huwa anapiga simu kupata taarifa kujua nini kinaweza kufanyika ili kuweka mambo sawa.

"Rais Samia angeweza kusema tu marufuku kupandisha bei za mafuta. Yeye ni Rais na anaweza kufanya chochote. Lakini aliamua kutafuta suluhisho la kudumu kwa kuwaita viongozi wa juu wa wizara na taasisi za serikali ambazo zinashughulika na masuala ya mafuta. Uamuzi huu umejengwa kwenye mwafaka wa viongozi," alisema mmoja wa viongozi waandamizi serikalini.

Kiongozi huyo alisema Rais alianza kushughulika na jambo hilo kuanzia Aprili, na Julai mwaka huu ndipo alipoagiza kufanyiwa kazi kwa suala hilo la bei ambalo hatima yake imefikiwa mwezi huu.

Miongoni mwa hatua kubwa zilizochokuliwa ni kwa serikali kukubali kupoteza mapato ya takribani Sh. bilioni 102 kwa mwaka zilizokuwa zikikusanywa kupitia tozo ili kushusha bei ya mafuta.

Sekta ya mafuta ilikuwa na tozo takribani 23 zilizokuwa zikichukuliwa na wizara na taasisi mbalimbali za serikali na zilikuwa ndiyo chanzo kikuu cha Tanzania kuwa na bei kubwa ya mafuta kuliko ile ambavyo ingetazamiwa.

Mmoja wa mawaziri wa Rais Samia aliyezungumza kwa masharti ya kutotajwa majina yake, alisema jambo kubwa ambalo wamejifunza katika ni kwamba Rais anafanya mambo yake kufuata ushauri wa wataalamu na hapendi kutumia cheo chake kulazimisha anachotaka.

"Mwanzoni kabisa tuliona kwamba alichokuwa anakitaka Rais Samia ni bei ya mafuta kushuka na alitaka wataalamu na mawaziri wao wakae chini kutengeneza namna ya kufikia hapo. Hakulazimisha bali alisikiliza na kutoa mapendekezo pale ilipobidi. Sote tumeridhika na tulipofika," alisema.

**SPIDI YA UTEKELEZAJI**

Siku ambayo Rais aliagiza kufanyiwa kazi kwa mapendekezo hayo ndiyo siku ambayo Waziri Makamba alitangaza kilichoamriwa na siku iliyofuata, EWURA wakatangaza bei mpya ya mafuta kutokana na marekebisho hayo.

Makamba pia alitoa tangazo kwenye Gazeti la Serikali siku hiyo hiyo na inatarajiwa kuwa katika Mkutano wa Bunge unaofuata Novemba mwaka huu, kuna uwezekano wa serikali kuleta mapendekezo zaidi ya kusaidia kushusha bei ya bidhaa hizo.

Utekelezaji huo umefanyika kwa kasi kubwa inayoonyesha kwamba sasa mifumo ya mawasiliano katika utawala wa Rais Samia imeanza 'kuonana' kama alivyowahi kusema Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga.

Mmoja wa wasomi na wachumi maarufu nchini, Profesa Samuel Wangwe, alipongeza hatua ya serikali ya Rais Samia kushughulika na suala la bei ya mafuta kwa sababu ni nyeti kiuchumi na athari zake ni mtambuka.

"Inapopanda bei ya mafuta, maana yake ni kwamba bei ya usafiri inapanda, bei ya bidhaa zinazosafirishwa inapanda, bei ya uzalishaji inapanda na gharama ya maisha kwa ujumla inapanda. Serikali imefanya vizuri kutafuta namna ya kuwaokoa wananchi na mzigo huo wa gharama," alisema.



# RIDHIWANI ATAKA STARS IPEWE USHIRIKIANO ZAIDI

**Na Somoe Ng'itu**

MBUNGE wa Jimbo la Chalinze (CCM), mkoani Pwani, Ridhiwani Kikwete amesema Tanzania (Taifa Stars), ina 'kiu' na ndoto ya kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zinazotarajiwa kufanyika mwakani nchini Qatar.

Ridhiwani alisema hayo juzi jioni wakati akiitakia matokeo mazuri Taifa Stars iliyokuwa kwenye maandalizi yake ya mwisho ya kuivaa Benin kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jana jioni.

Mbunge huyo alisema kwa Tanzania huu ni wakati muhimu wa kuhakikisha wanashirikiana vyema na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), ili kufikia kwenye malengo ya kitaifa.

"Kwangu mimi mechi hii (Benin),ni muhimu sana, sisi kwetu ni zaidi ya kupata ushindi, ni kipindi kirefu tumekuwa na hamu ya kushiriki fainali hizo, jukumu letu ni kuendelea kuwatia moto, kuwatakia kila la kheri vijana wetu, wajiamini wanaweza," alisema Ridhiwani.

Aliongeza hatua ambayo Taifa Stars wamefikia ni kubwa na kila mmoja anatakiwa kuongeza ushirikiano kwa TFF, benchi la ufundi na wachezaji ili kutimiza ndoto. "Ni jukumu letu kuwatia moyo viongozi wetu, benchi la ufundi, vijana wetu waamini wanaweza, waamini nchi iko pamoja nao," Ridhiwani aliongeza.

Naye Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema hatua ambayo Taifa Stars imefikia mwaka huu ni ya kujivunia, hivyo jitihada za pamoja zinahitajika ili wawakilishi wetu waendelee kufanya vyema kwenye michuano hiyo.

Kabwe alisema hatua ambayo Taifa Stars imefikia ni kubwa na kila mmoja anaitakia mafanikio kwenye mechi zake zote zinazofuata.

"Endapo Tanzania itafanikiwa kuwafunga Benin kesho (jana), basi itaendelea kuongoza kundi kwa mbali kwa sababu itawapita hao Benin pointi tatu, sasa hivi wanalingana pointi, lakini Taifa Stars inabebwa na faida ya magoli ya kufunga," alisema Kabwe.

Taifa Stars ilianza kampeni ya kuelekea Qatar kwa kutoka suluhu na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ugenini na ikaifunga Madagascar mabao 3-2 hapa nyumbani.

Baada ya mechi ya jana, Taifa Stars itasafiri kuwafuata Benin kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaochezwa Oktoba 12, mwaka huu jijini Cotonou.




Mkurugenzi wa Shule ya Atlas iliyoko Madale, Sylivanus Rugambwa (kulia), akizungumza kuhusu maandalizi ya mbio za nusu marathon zitakazofanyika Oktoba 14, mwaka huu, ambazo lengo lake ni kusaidia wanafunzi zaidi ya 200 wa shule hiyo, wanaosomeshwa bure kutokana na sababu mbalimbali. Katikati ni Ofisa Habari wa Atlas, Lenarda Philbert na Katibu wa Chama cha Riadha Dar es Salaam, Rahim Kalyango . **PICHA: MIRAJI MSALA**

# M-Bet yamwaga mil. 961/-, shabiki Yanga ashinda milioni 104.3/-

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya mchezo ya kubashiri ya M-Bet Tanzania imetumia jumla ya Sh milioni 961 kuzawadia washindi mbalimbali wanaobashiri kwa usahihi matokeo ya ligi mbalimbali duniani kupitia mchezo wa Perfect 12 na Jackpot Bonus.

Hayo yalisemwa na Meneja Masoko wa kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi wakati wa kumzawadia zawadi yake Stephano Ndunguru kutoka mkoani Njombe aliyeshinda Sh. milioni 104.3.

Mushi alisema kuwa Ndunduru anakuwa mshindi wa 10 kuzawadiwa mamilioni ya fedha kwa mwaka huu na kuifanya kampuni yao kutumia kiasi hicho cha fedha.

Alisema kuwa wanajisikia faraja sana kuendelea kubadili na kuwawezesha wanamichezo kupitia michezo yao ya kubashiri na sasa kuwa na maisha bora.

"Mbali ya kubadili maisha ya washindi wetu kupitia kubashiri michezo, pia tunajisikia fahari kuchangia asilimia 20 ya kodi ya ushindi ambayo inaigia moja kwa moja serikalini . Sisi ni walipa kodi wazuri wa serikali na tunachangia maendeleo," alisema Mushi.

Alisema kuwa kati ya fedha hizo, Sh milioni 791 ni zawadi za moja kwa moja kwa washindi wakati Sh. milioni 200 ni zawadi kwa ya 'jackpot' bonus. Alisema kuwa wanatarajia kuwazadia washindi wengi mwaka huu kwani ligi mbalimbali zinaendelea mpaka sasa.

Kwa upande wake, Ndunduru ambaye ni shabiki wa Yanga alisema kuwa hakuamini kushinda kiasi hicho cha fedha kwa kutumia Sh1, 000 tu. "Mimi mkulima wa maharagwe, nimekuwa nikibashiriki na kupata hela ndogo ndogo. Nilipopigiwa simu na kuambiwa kuwa nimeshinda zaidi ya milioni 100, sikuamini na nilidhani ni ndoto," alisema Ndunduru.

Alisema kuwa fedha hizo atazitumia kuendesha kilimo cha kisasa zaidi na kutoa ajira kwa watu wengine.

## Mil. 40/- kushindaniwa CRDB Bank Taifa Cup

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU 32 za mikoa za mpira wa kikapu zinatarajiwa kuchuana vikali katika mashindano ya CRDB Bank Taifa Cup yanayotarajiwa kufanyika katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma kuanzia Novemba 5 hadi 14 mwaka huu.

Akitangaza zawadi hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kuongezeka kwa zawadi katika CRDB Bank Taifa Cup mwaka huu kunatokana na kuongeza udhamini wa benki hiyo katika mashindano hayo kufikia shilingi milioni 300.

"Tumeona tuongeze zawadi mwaka huu ili kuongeza ushindani kwa timu na vijana watakaoshiriki. Tunaamini kuongezeka kwa zawadi kutakuwa na motisha kwa vijana kuonyesha vipaji vyao," alisema Nsekela.

Nsekela alisema Benki ya CRDB imeendelea na uamuzi wake wa kudhamini ligi hiyo ya taifa ya mpira wa kikapu kwa mara ya pili mfululizo ikiwa ni sehemu ya jitihada za benki hiyo kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupitia michezo.

## Tuzo za digitali msimu mpya zaja

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa Tuzo za Digitali (Tanzania Digital Awards) mwaka 2021 umezinduliwa rasmi jana jijini Dar es Salaam zikiwa zinakusudia kukuza uwajibikaji, ubunifu, na uvumbuzi katika uwanda wa digitali Tanzania.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi jijini Dar es Salaam Ofisa Uendeshaji wa Kampuni ya Serengeti Byte, Michael Mallya, ambao ni waandaaji wa tuzo hizo alisema wanatarajia msimu wa kusisimua na kuwa wenye ushindani zaidi.

Alisema Taasisi za umma, makampuni, mashirika yasiyo ya kiserikali, na watu binafsi walipendekezwa na kupigiwa kura katika vipengele 10.

Alivitaja vipengele vilivyowaniwa mwaka jana ni pamoja na Serikali Mtandaoni, Diplomasia Mtandaoni, Masoko Mtandao, Burudani Mtandaoni, Vyombo vya Habari Mtandaoni, Uvumbuzi wa Kidijitali, Mawasiliano ya Kidijitali, Uchechemuzi Mtandaoni, Tuzo ya Heshima na Tuzo ya Ujumla ya Chaguo la Watu.

"Kufuatia maoni ya wadau mbalimbali, mwaka huu Tanzania Digital Awards imepanua wigo kwa kuongeza idadi ya vipengele vikuu kuwa 12 na vipengele vidogo 52," alisema.

Mallya alisema vipengengele vikuu vya mwaka 2021 ni pamoja na Uvumbuzi wa Kidijitali, Huduma za Benki Kidigitali, Sekta ya Mawasiliano ya Simu Kidigitali, Mawasiliano Kidigitali, Burudani Kidigitali, Masoko na Biashara Kidigitali, Vyombo vya Habari Kidigitali, Serikali Kidigitali, Uchechemuzi Kidigitali, Diplomasia Kidigitali, Tuzo ya Chaguo la Watu na Tuzo ya Heshima,

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YALENGA WAWILI
ARSENAL wanawalenga wachezaji wawili wa England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 24 na Ollie Watkins mwenye miaka 25, lakini inakabiliwa na kibarua kigumu kuwatoa kule Everton na Aston Villa. **(Sun)**

### TEZGEL ATAKIWA
KLABU ya Manchester City, Chelsea na Manchester United wanajiandaa kumwania mshambuliaji kinda wa Stoke City, Emre Tezgel mwenye miaka 16, ambaye amekuwa akifananishwa na Harry Kane. **(Mail)**

### WIRTZ AGOMBEWA
KLABU za Ligi Kuu ya England ya England vitapambana na Bayern Munich kumnasa kiungo wa kati wa Ujerumani, Florian Wirtz anayekipiga Bayer Leverkusen. **(Fabrizio Romano)**

### VLAHOVIC ATAKIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL wanafikiria uhamisho wa mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, ambaye mazungumzo kuhusu mkataba yamevunjika Fiorentina. **(Mirror)**

### LANG AWANIWA
ARSENAL bado wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Club Bruges, Noa Lang mwenye umri wa miaka 22, na AC Milan pia inavutiwa naye.**(Calciomercato, via TEAMtalk)**

### HALAANAD KUBAKI
KLABU ya Borussia Dortmund imeamua kubaki na mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 hadi mwaka 2023.**(Sport Bild)**

### WINKS KUONDOKA
KIUNGO wa kati wa England na Tottenham Hotspur, Harry Winks mwenye umri wa miaka 25, anataka uhamisho wa mkopo kutoka kwenye klabu hiyo Januari na yuko radhi kwenda nje ya England. **(Times - subscription required)**

### MBAPPE NA MUSTAKABALI
MUSTAKABALI wa muda mrefu wa nyota wa Ufaransa, Kylian Mbappe bado utategemea Paris St-Germain baada ya mazungumzo kati ya mama wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, kukubaliana na mabingwa hao Ufaransa kuhusu mkataba mpya kwenda vizur**i.(RMC via AS)**

### UMTITI KUUZWA
BARCELONA itamfanya beki wa Ufaransa, Samuel Umtiti apatikane Januari hii. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hajacheza hata dakika moja katika ligi ya LaLiga msimu huu. **(Sport)**

### ONANA KUTUA INTER
GOLIKIPA wa Ajax na Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25, yuko tayari kujiunga na Inter Milan kama mchezaji huru mwaka 2022. (Fabrizio Romano)

### XAVI KUMRITHI KOEMAN
BARCELONA imeendelea na mazungumzo na kiungo wa kati wa zamani, Xavi mwenye umri wa miaka 41 ili achukue nafasi ya kocha, Ronald Koeman, lakini makubaliano na raia huyo wa Hispania hayajafikiwa. **(90min)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI: SIKUFANYA MAKOSA KUONDOKA BARCELONA

●●● Asema lilikuwa jambo la lazima na sasa anafurahia kuanza maisha mapya na...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi amesisitiza kuwa hakufanya kosa kuondoka klabu yake ya utotoni, Barcelona kwenda kwa miamba ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain.

Messi alijiunga na PSG kwa uhamisho huru baada ya Barca kushindwa kumwongezea mkataba mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or kutokana na matatizo ya kifedha.

Uhamisho huo ulimaliza muda wa Messi kukaa pale Barca, akiwa ameanza kuwachezea miamba hao wa LaLiga kwa mara ya kwanza msimu wa 2004-05.

Messi alishinda mataji 35 akiwa pale Camp Nou, akifunga mabao 672 katika mashindano yote.

Na sasa ameanza maisha mapya na PSG, na Messi amesema ana furaha kutokana na maamuzi yake hayo.

"Sikufanya makosa kwenda PSG," amesema Messi akiliambia jarida la France Football katika mahojiano maalumu ambayo yatachapishwa Jumamosi.

Tangu kuhamia PSG, Messi amefunga bao moja tu katika klabu hiyo kwenye ushindi wa 2-0 katka Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 bado hajafunga bao kwenye Ligi Kuu ya Ligue 1, na PSG walifungwa mabao 2-0 na Renne wiki iliyopita.

PSG imeanza vizuri msimu huu ikishinda mechi nane mfululizo, huku kikosi hicho cha Messi kikiongoza msimamo wa Ligi kwa pointi sita baada ya mechi tisa.

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 559

MECHI KALI
HOME AWAY
MALAWI
8.53 | 4.46 | 1.33
IVORY COAST

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# POGBA ATAKA ALIPWE BIL 1.2 KWA WIKI

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba amewaambia watu wake wa karibu kuwa anataka kuongeza mkataba wake Manchester United huku Real Madrid, Juventus na Paris Saint-Germain zikionyesha nia ya kumsajili.

Mkataba wa sasa wa Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 28 unamalizika msimu ujao.

Hata hivyo, ripoti kutoka Ufaransa zinasema Pogba ameamua kubaki United na sasa hafichi kuhusu ukweli huo.

Kwa mujibu wa ripoti hizo United inataka mkataba mpya wa Pogba ukamilike ifikapo sikukuu ya Krimasi na amekuwa katika majadiliano ya mara kwa mara wakala wake Mino Raiola.

Masharti ya mkataba mpya yatampatia Pogba mshahara wa pauni 400, 000 sawa na shilingi bilioni 1.2 kwa wiki.

Iliripotiwa kuwa PSG ina nia ya kumpa ofa Pogba ya mshahara wa pauni 510,000 sawa na shilingi bilioni 1.5 kwa wiki iwapo itamsajili akiwa mchezaji huru.



# Mrithi wa Lacazette asakwa

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Atreta alisema imeanza kuwatambua mastraika ambao itahitaji kunasa saini zao ikiwa ni maandalizi ya kuachana na Alexandre Lacazette.

Nyota wa kimataifa wa England, Dominic Calvert-Lewin wa Everton na Ollie Watkins wa Aston Villa wanatajwa kuwapo kwenye orodha ya wachezaji wanaosakwa na Arsenal kwenda kuchukua mikoba ya Lacazette.

Lacazette mwenye umri wa miaka 30, yupo kwenye mwaka wa mwisho wa mkataba wake wenye thamani ya pauni 180,000 kwa wiki na hajapewa ofa yoyote ya mkataba mpya.

Kuna uwezekano mkubwa wa Arsenal ikafungua milango ya kumpiga bei kwenye dirisha la uhamisho wa Januari, wakiepuka kumpoteza bure kabisa mwishoni mwa msimu. Lakini, Kocha Mikel Arteta ataruhusu hilo kutokea kama tu ataweza kusaini mshambuliaji mwingine wa kusaidiana na Pierre-Emerick Aubameyang.

Baada ya kutumia pauni milioni 148 kusajili wachezaji sita kwenye dirisha lililopita la uhamisho wa majira ya kiangazi, Arsenal wamepanga kufanya usajili mwingine Januari mwakani.

Lacazette, aliyenaswa kwa pauni milioni 52 akitokea Lyon mwaka 2017, hajaanzishwa kwenye mechi yoyote ya Ligi Kuu England msimu huu baada ya kupata maambukizi ya Uviko 19 siku moja kabla ya kuanza kwa msimu huu.

Kwenye kikosi cha Arsenal, yeye ndiye mshambuliaji pekee mwenye uzoefu ukimweka kando Aubameyang, hivyo kama ataondoka ataacha pengo ambalo Arteta atakuwa na shughuli kubwa ya kuliziba.

Hata hivyo, washambuliaji Calvert-Lewin, 24, na Watkins, 25, ambao Arteta anawataka wote wapo na mikataba mirefu kwenye timu zao, itakayofika tamati 2025, hivyo saini zao haziwezi kupatikana kwa gharama nafuu.

## HABARI MICHEZO


# 9,183,880

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/10/21 | 17:00 | Lugo vs Girona | 2.95 | 2.95 | 2.51 |
| 02. 09/10/21 | 17:00 | Hartlepool vs Northampton | 2.55 | 2.99 | 2.84 |
| 03. 09/10/21 | 17:00 | Bristol Rovers vs Carlisle | 2.55 | 3.09 | 2.75 |
| 04. 09/10/21 | 17:00 | Stevenage vs Exeter | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 05. 09/10/21 | 17:00 | Sutton United vs Port Vale | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 06. 09/10/21 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 09/10/21 | 17:00 | Newport vs Bradford City | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 08. 09/10/21 | 17:00 | Boreham Wood vs Dagenham and Redbridge | 2.49 | 3.22 | 2.68 |
| 09. 09/10/21 | 22:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.70 | 2.94 | 2.75 |
| 10. 10/10/21 | 08:00 | Matsumoto Yamaga vs Tochigi SC | 2.61 | 2.86 | 2.76 |
| 11. 10/10/21 | 15:00 | Real Sociedad B vs Ponferradina | 2.56 | 3.00 | 2.85 |
| 12. 10/10/21 | 19:15 | Alcorcon vs Burgos | 2.57 | 3.02 | 2.82 |
| 13. 10/10/21 | 22:00 | Fuenlabrada vs Leganes | 2.63 | 2.88 | 2.88 |


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 08 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4387 | Malawi vs Ivory Coast | 8.53 | 4.46 | 1.33 |
| 16:00 | 5154 | Fastav Zlin B vs Sigma Olomouc B | 4.26 | 4.35 | 1.59 |
| 18:00 | 1789 | RoPs Rovaniemi vs EIF Ekenas | 1.60 | 4.17 | 4.36 |
| 18:00 | 1821 | Shabab Alsamu vs Jabal EL Mokaber | 3.43 | 3.24 | 2.02 |
| 18:00 | 2151 | Moldova U21 vs Wales U21 | 3.53 | 3.15 | 2.02 |
| 18:30 | 1251 | Lithuania U21 vs Malta U21 | 1.56 | 3.82 | 5.22 |
| 18:30 | 1587 | TPS Turku vs VPS Vaasa | 1.57 | 3.73 | 5.24 |
| 18:30 | 1605 | Bulgaria U21 vs Gibraltar U21 | 1.01 | 13.58 | 48.51 |
| 18:30 | 2757 | Bosnia and Herzegovina U21 vs Italy U21 | 6.38 | 4.54 | 1.39 |
| 19:00 | 1561 | Belarus U21 vs Greece U21 | 5.22 | 3.72 | 1.58 |
| 19:00 | 1684 | Russia U21 vs Northern Ireland U21 | 1.31 | 4.87 | 7.79 |
| 19:00 | 2108 | Sweden U21 vs Montenegro U21 | 1.28 | 5.04 | 8.72 |
| 19:00 | 2568 | Angola vs Gabon | 2.21 | 2.86 | 3.40 |
| 19:00 | 3022 | Cameroon vs Mozambique | 1.17 | 5.78 | 15.42 |
| 19:00 | 3033 | Croatia U21 vs Norway U21 | 1.67 | 3.76 | 4.34 |
| 19:15 | 3926 | Ireland U21 vs Luxembourg U21 | 1.08 | 8.13 | 20.32 |
| 19:30 | 1420 | Azerbaijan U21 vs Finland U21 | 3.74 | 3.54 | 1.83 |
| 19:30 | 1722 | France U21 vs Ukraine U21 | 1.39 | 4.35 | 6.77 |
| 20:00 | 1388 | Cornella vs Real Madrid Castilla | 2.57 | 3.15 | 2.57 |
| 20:00 | 2182 | Cholet vs Orleans | 2.58 | 3.22 | 2.58 |
| 20:00 | 2736 | Avranches vs Red Star | 2.59 | 3.18 | 2.59 |
| 20:00 | 3769 | Chateauroux vs Concarneau | 2.08 | 2.99 | 3.72 |
| 20:00 | 3773 | Bastia Borgo vs Annecy FC | 3.86 | 3.13 | 1.97 |
| 20:00 | 4403 | Estonia U21 vs Austria U21 | 38.75 | 11.62 | 1.02 |
| 20:00 | 4852 | Athletic Bilbao B vs Celta B | 2.11 | 3.10 | 3.34 |
| 20:00 | 5298 | Sete 34 FC vs Laval | 2.93 | 2.93 | 2.49 |
| 20:00 | 5515 | Creteil vs Boulogne | 2.83 | 2.97 | 2.53 |
| 20:00 | 5582 | Switzerland U2 vs Netherlands U21 | 3.15 | 3.34 | 2.09 |
| 20:00 | 5594 | Le Mans vs Chambly | 1.83 | 3.27 | 4.30 |
| 20:00 | 5600 | Saint Brieuc vs Villefranche Sur Saone | 2.99 | 2.85 | 2.50 |
| 21:00 | 1189 | Belgium U21 vs Kazakhstan U21 | 1.03 | 10.72 | 29.25 |
| 21:00 | 1702 | Hungary U21 vs Poland U21 | 2.95 | 3.34 | 2.19 |
| 21:45 | 1139 | Tranmere vs Colchester | 2.10 | 3.09 | 3.58 |
| 21:45 | 1700 | Germany vs Romania | 1.16 | 7.19 | 17.10 |
| 21:45 | 2023 | Iceland vs Armenia | 2.17 | 3.25 | 3.44 |
| 21:45 | 2166 | Czech Republic vs Wales | 1.70 | 3.59 | 5.19 |
| 21:45 | 2358 | Latvia vs Netherlands | 24.94 | 9.98 | 1.09 |
| 21:45 | 2499 | Estonia vs Belarus | 2.36 | 3.15 | 3.15 |
| 21:45 | 3102 | Liechtenstein vs North Macedonia | 21.00 | 7.40 | 1.14 |
| 21:45 | 3586 | Turkey vs Norway | 2.18 | 3.35 | 3.30 |
| 21:45 | 3671 | Cyprus vs Croatia | 13.03 | 5.41 | 1.25 |
| 21:45 | 3868 | Russia vs Slovakia | 1.83 | 3.39 | 4.59 |
| 21:45 | 4870 | Malta vs Slovenia | 7.80 | 3.90 | 1.48 |
| 21:45 | 4937 | Gibraltar vs Montenegro | 20.90 | 9.35 | 1.10 |
| 21:45 | 5000 | Spain U21 vs Slovakia U21 | 1.14 | 6.96 | 13.52 |
| 21:45 | 5487 | Dundalk FC vs Shamrock Rovers | 3.10 | 3.20 | 2.17 |
| 22:00 | 3309 | Algeria vs Niger | 1.07 | 8.32 | 23.21 |
| 22:00 | 4198 | Egypt vs Libya | 1.27 | 4.74 | 10.63 |
| 22:00 | 5309 | Valladolid vs Malaga | 1.90 | 3.25 | 4.14 |
| 23:00 | 1819 | Djibouti vs Burkina Faso | 29.21 | 13.63 | 1.01 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ROY KEANE AIPA UBINGWA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, ametoa utabiri wake wa timu gani itakayobeba ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu na chaguo lake ni kikosi cha kocha Pep Guardiola, Manchester City.

Man City ililazimisha sare ya 2-2 dhidi ya Liverpool kwenye uwanja wenye kelele nyingi za mashabiki Anfield, baada ya Phil Foden na Kevin de Bruyne kuchomoa mabao ya wakali wa Liverpool, Sadio Mane na Mohamed Salah.

Hata hivyo, Keane hakuisahau timu yake ya zamani ya Man United, ambapo alikuwa nahodha huko Old Trafford, kwamba watamaliza ligi ndani ya nne bora.

Msimamo ulivyo kwa sasa, Chelsea inaongoza ikiwa na pointi 16, wakati Liverpool ipo kwenye nafasi ya pili na pointi zao 15, huku Man City kwenye nafasi ya tatu na Man United namba nne na pointi zao 14 kila mmoja.

Keane alisema timu hizo nne zitafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, lakini anaamini vijana wa Guardiola watatetea taji lao kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Kiungo huyo gwiji aliiambia Sky Sports: "Ukitazama msimamo, unaona kabisa Top Four ilivyo.

"Kama utawafanyia uchambuzi Liverpool, unaona wiki iliyopita waliruhusu mabao matatu dhidi ya Brentford na wikiendi hii wameruhusu mabao mawili, hiyo sio dalili nzuri.

"Lakini, wana wachezaji wazuri sana kwenye fowadi yao, washambuliaji wa kiwango cha dunia.

"Lakini, naamini timu hizi ikiwamo na Chelsea, zinaweza kufanya vizuri na kumaliza ligi juu ya Man City."



# Hispania yatinga fainali Uefa

**MILAN, Italia**

MABINGWA wa Euro 2021, Italia wameshindwa kutinga fainali ya michuano ya Uefa Nations League 'baada ya kufungwa 2-1 na Hispania kwenye mchezo uliocheza usiku wa kuamkia jana katika dimba la San Siro.

Mabao ya Hispania yalifungwa na Ferran Torres dakika ya 17 na 45 kabla ya kwenda mapumziko huku ikishuhudiwa nahodha wa mchezo huo beki Leonardo Bonucci akioneshwa kadi nyekundu dakika ya 42 kabla ya Lorenzo Pellegrini kufunga bao dakika 83 la kufutia machozi kwa Italia.

Kipigo hiko kimewafanya Hispania kuvunja rekodi ya Italia ya kucheza michezo 37 mfululizo ya michuano yote bila kufungwa.

Pia, Italia imefungwa kwa mara ya kwanza kwenye mchezo rasmi kwenye uwanja wake wa nyumbani tangu mwaka 1999 wakati ambao wachezaji makinda wa Hispania sita waliokuwa kwenye mchezo huo waliokuwa hawajazaliwa ambao ni Pedro Porro, Ferran Torres, Eric Garcia, Bryan Gil, Yeremia Pino na Gavira 'Gavi'.

Kwa upande mwingine, Hispania imezidi kuonesha ubabe wake mbele ya Italia, kwani ilikuwa ni mchezo wao wa 34, Hispania wakishinda michezo 12, Italia ikishinda 10 na wakitoa sare mara 12.

Michezo
Ijumaa Oktoba 8, 2021
Nipashe



Messi: Sikufanya makosa kuondoka Barca

UKURASA 21



Nahodha wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, Mbwana Samatta (kushoto), akimtoka mlinzi wa Benin kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia uliopigwa jana, Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Stars ilifungwa bao 1-0. **PICHA; MTANDAO**

# STARS YAZIMWA, TWIGA YATAKATA

●●●Sasa yashushwa hadi nafasi ya tatu kwenye kundi, Congo ikipaa nafasi ya pili...

**Na Adam Fungamwangko**

HUKU ikikosa mabao mengi ya wazi, timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars jana ilipoteza mechi yake ya kwanza ya kusaka tiketi kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Benin.

Alikuwa ni straika anayechezea klabu ya Stade Brestois ya Ufaransa, Steve Mounie aliyewanyamazisha Watanzania wapatao 10,000 waliohudhuria mechi hiyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, alipofunga bao kwa shuti la kiufundi la staili ya 'mwezi mwandano', baada ya kupokea pasi ndefu kutoka winga ya kushoto.

Straika huyo aliwahadaa mabeki wa Stars kabla ya kupiga shuti hilo, pamoja na kipa Aishi Manula kujinyoosha hadi mwisho kutaka angalau aguse tu kuupoteza mwelekeo, lakini akishuhudia mpira ukitinga wavuni dakika ya 71.

Ilikuwa ni baada ya mlolongo wa wachezaji wa Stars kukosa mabao ya wazi, huku kipa Saturnin Allagbe akiwa kikwazo kwa mastraika wa Tanzania ambao karibuni wote walikosa mabao ya wazi.

Dakika ya 11 kilitokea kizaazaa kwenye lango la Benin, lakini shuti la Feisal Salum liliwababatiza mabeki wa kuwaweka salama wageni.

Simon Msuva angeweza kabisa kuipatia Stars bao dakika ya 18, lakini aliukosa mpira na kupiga hewa, kufuatia krosi maridadi iliyochongwa na nahodha Mbwana Samatta.

Msuva tena, aliwashangaza watazamaji waliohudhuria mechi hiyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na waliokuwa wakifuatilia kwenye televisheni, alipompiga chenga ya kichwa kipa wa Benin na kubaki yeye na nyavu, lakini akapiga shuti dhaifu ambalo akidhani linatinga wavuni, liliokolewa na beki wa Benin na kusababisha masikitiko kwa Watanzania.

Benin ilifanya shambulizi la kushtukiza kwenye lango la Stars dakika ya 25, baada ya Desire Azankpo kuachia shuti kali akiwa umbali ya mita 30, lakini lilitoka juu ya lango.

Manula aliiokoa Tanzania alipodakia shuti la ana kwa ana akiwa na Yossoug Assouba dakika ya 35.

Pamoja na kufanya mabadiliko kipindi cha pili, hali ikawa ni vile vile.

Stars ambayo ilikuwa ikiongoza kundi J kwa pointi nne imeteremka mpaka nafasi ya tatu, ikisalia na pointi zake hizo, huku Benin ikipaa hadi kufikisha pointi saba, wakati huo Jamhuri ya Congo (DRC) ikipanda hadi nafasi ya pili kwani ikiwa nyumbani jana, ilichapa Madagascar mabao 2-0. Madagascar inashika mkia ikiwa haina pointi hata moja.

Wakati huo huo, Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake Twiga Stars, imefanikiwa kutinga hatua ya fainali ya michuano ya wanawake Ukanda wa Kusini mwa Afrika COSAFA kwa kuiondoa Zambia kwa mabao 3-2 yaliyopatikana kwa mikwaju ya penalti kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Bay, nchini Afrika Kusini.

Timu hizo zililazimika kupigiana penalti baada ya sare ya bao 1-1 kwa dakika 90 za mchezo.

Twiga ambao ni wageni waalikwa, watacheza na mshindi kati ya Afrika Kusini na Malawi, ambao walitarajia kucheza mechi ya pili ya nusu fainali.

## Yanga, Azam kukipiga Arusha

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umeiandikia barua Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) kuomba mchezo wake namba 31 wa mzunguko wa nne wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC uchezwe kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Awali kwenye ratiba ya Bodi ya Ligi mchezo huo ulipangwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam huku Yanga wakiwa wenyeji.

Ofisa habari wa Yanga, Hassan Bumbuli akizungumza jijini Dar es Salaam jana, alisema kuwa wameomba mchezo huo kwenda kuchezwa Arusha kwa ajili ya kuwapelekea burudani mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

"Mashabiki na wanachama wa Yanga wa mkoa wa Arusha na mikoa jirani wanahamu kubwa na timu yao, lakini mashabiki wa soka kiujumla katika ukanda wa mikoa ya kaskazini wanashauku kushuhudia mchezo mkubwa, hivyo kwa kuwajali tumeandika barua kwa Bodi ya Ligi kuomba mchezo wetu na Azam uchezwe Arusha na tuna imani tutakubaliwa ombi letu," alisema Bumbuli.

Taarifa hiyo ilithibitishwa na Ofisa Habari wa TPBL, Karim Boimanda, ambaye alikiri bodi hiyo kupokea barua ya maombi ya klabu ya Yanga.

" Ni kweli barua ya Yanga imefika jana (juzi) taratibu nyingine zinaendelea kabla ya kuwajibu..., kwa sasa itoshe kusema ni kweli barua tumeipata," alisema Boimanda.

Alisema Bodi ya Ligi inaifanyia kazi barua hiyo na baada ya kumaliza watawajulisha Yanga juu ya maombi yao hayo.

Katika hatua nyingine, uongozi wa Yanga umemua kufutilia mbali mpango wao wa kwenda kuweka kambi mkoani Arusha kujiandaa na mchezo wao dhidi ya KMC uliopangwa kuchezwa mjini Songea.

Yanga wameamua kufuta mpango huo kwa kile wanachodai mwingiliano wa majukumu ya baadhi ya wachezaji wao waliopo kwenye kikosi cha timu ya taifa 'Taifa Stars'.

Bumbuli, alisema wmeona watawachosha zaidi wachezaji wao hao hivyo wameamua timu iendelee kuweka kambi jijini Dar es Salaam na baadaye wataenda kuweka kambi Arusha kujiandaa na mchezo dhidi ya Azam kama maombi yao ya kucheza mchezo huo Arusha yatakubaliwa na Bodi ya Ligi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042